SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**WAFUKUA** kaburi la mwenye ualbino, waondoka na viungo

UKURASA 3




UKURASA 11

Jumatatu Novemba 1, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580751

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Tanzania kupata mabilioni mabadiliko ya tabianchi

UKURASA 2



Eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam likiwa wazi kutokana na wafanyabiashara wadogo 'Machinga' kuondoa vibanda vyao jana, ili kutii agizo la serikali la kuhama katika maeneo hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Spika Ndugai akerwa Bunge kuaibishwa

UKURASA 2




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akitangaza ripoti ya ukuaji mkubwa katika matokeo yake ya fedha ya robo ya tatu ya mwaka iliyoishia Septemba 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam. Katika ripoti hiyo iliyotangazwa mwishoni mwa wiki, Benki ya CRDB iliripoti ongezeko la 39.9% ya Faida Kabla ya Kodi kufikia Sh. bilioni 238 ikilinganishwa na Sh. bilioni 170 iliyorekodiwa mwishoni mwa robo ya tatu ya 2020. **Habari UK. 3**. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Mnada wa korosho wasitishwa kukosekana kampuni za ununuzi

UKURASA 4

MICHEZO NABI ATANGAZA SOKA 'SAMBUSA' BADO YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Megawati 1,100 nishati jadidifu kuzalishwa nchini

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema ifikapo 2025 itazalisha megawati 1,100 za nishati jadidifu kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi ili kuongeza upatikanaji wa umeme kwa wananchi wa kawaida na sekta mbalimbali.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Felschemi Mramba, wakati akifunga mafunzo ya wiki moja kwa waandishi wa habari yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la madini, mazingira na afya ya wananchi (HAKIMADINI). Alisema mikakati iliyopo kwa sasa ifikapo 2023 uzalishaji ufikie megawati 550 ambayo sekta binafsi ni kuzalisha 400 na TANESCO 150, ifikapo 2025 zizalishwe 600 ikiwamo 200 zitokanazo na joto ardhi.

Alisema uzalishaji wa umeme kwa sasa nchini unaotokana na maji ni megawati 1,605, gesi ni 900 na maji 508 huku nishati jadidifu ikizalisha 58, na kwamba msukumo mkubwa ni kuongeza nishati hiyo. Nishati jadidifu huzalishwa kutokana na jua, upepo, joto ardhi na mimea na hadi sasa zipo kampuni zinazozalisha umeme na kuuza kwa wananchi moja kwa moja na mwingine ukitumika viwandani.

Alisema Tanzania imejaliwa nishati ya jua na umeme kwa wingi na tayari utafiti umefanyika kwenye mikoa ya Mbeya, Songwe, Singida, Shinyanga na Dodoma ambako kuna uwezekano mkubwa wa kuzalisha nishati hiyo.

"Tuna umeme wa jua mwingi sana, pia upepo upo wa kutosha na bado utafiti umeonyesha maeneo yanayofaa kuzalisha nishati kwa joto ardhi, ni wakati sasa wa kutumia kwa kuwa wakati mwingine ni gharama kubwa sana kupeleka umeme wa TANESCO kwenye eneo fulani, lakini kukiwa na wawekezaji wanaozalisha huko huko wanawauzia wananchi," alisema Mramba.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wanatumia nishati ya mimea yaani mkaa au kuni ambayo kwa kiasi kikubwa inachangia uharibifu wa mazingira, huku asilimia nane hadi 10 wanatumia umeme na ndiyo maana nguvu kubwa inaelekezwa kwenye kuzalisha nishati jadidifu.

Naye Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ruft Valler inayosambaza umeme kwenye zaidi vijiji 20 na kuiuzia TANESCO, Deo Massawe, akiwasilisha mada ya shughuli wanazofanya, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza usumbufu na utitiri wa vibali kwa wawekezaji.

Naye Mjiolojia John Bosco Tindyebwa, akiwasilisha mada ya hali ya nishati jadidifu nchini na duniani, alisema bado kuna kikwazo kwenye sera, sheria na kukosekana mamlaka ya udhibiti inayosimamia nishaati jadidifu kwa kuwa zilizopo zimetaja nishati kwa ujumla wake.

# Tanzania kunufaika mabilioni ya tabianchi

**Na Waandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kuwa miongoni mwa nchi zitakazonufaika na mabilioni ya fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadilio ya tabia nchi.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameshawasili Glasgow nchini Scotland, anatarajia kuhutubia katika mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa (COP 26) utakaojadili mabadiliko ya tabia nchini ulioanza leo utakaowaleta pamoja wakuu wa nchi na serikali 130.

Pia, Rais Samia atakutaka na Mjumbe maalum wa Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson kwa ajili ya mazungumzo.

Hayo yalisemwa jana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Iringa kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini.

"Na tayari viongozi hao walishakubaliana kwamba nchi kubwa zitatoa pesa dola za Marekani bilioni 100 ambazo zitagawiwa kwenye baadhi ya nchi kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko hayo na Tanzania itakuwamo katika mgao huo. Miongoni mwa kazi ambayo pesa hiyo itafanya ni pamoja na kupanda misitu kukabiliana na mmonyoko wa ardhi na hatua nyinginezo."

"Nchi yetu imeridhia itifaki mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, kwa hiyo ndiyo maana sisi tunashiriki ili kuungana na nchi nyingine duniani juu ya namna mbalimbali za mabadiliko hayo," alifafanua Msigwa.

Kwa mujibu wa Msigwa, Rais Samia pia atakutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Shirika la GCF ambalo limetoa fedha kwa benki ya CRDB kwa ajili utekelezaji wa miradi ya kilimo.

Alisema mkutano mwingine ambao Rais Samia anatarajia kushiriki ni wa viongozi wanawake ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa (UN).

"Kwa hiyo Rais wetu hajakwenda kutembea, amekwenda kutuhangaikia," alisisitiza.

**KIKOKOTOO**

Msemaji huyo alisema "Serikali inaendelea kutafakari jambo hilo kwa kushirikiana na vyama vya wafanyakazi tuone namna bora ya kufanya na wakati ukifika mtajulishwa, lakini kwa sasa kila mfanyakazi anaendelea na vikokotoo vile vile hakuna kilichobadilika na mafao yanaendelea kutolewa kama kawaida."

"Na wanaostaafu wanapata mafao yao kwa wakati isipokuwa kwa wale wanaopata matatizo ni kwa sababu taarifa zao zinakuwa zinarekebishwa," aliongeza.

**CHANJO MPYA YA UVIKO-19**

Aidha, Msigwa alisema leo serikali inapokea dozi nyingine 500,000 aina ya Sinopharm kutoka China, na kwamba chanjo 500,000 aina ya Pfizer italetwa wakati wowote.

**MAWAZIRI KUZUNGUMZA**

Msigwa alisema katika kuelekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika, kuanzia leo viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri watakuwa wanazungumza na vyombo vya habari kueleza mambo mbalimbali ya sekta zao.

Alisema katika kuhakikisha TEHAMA inakua nchini, serikali imeamua kuondoa kodi ili kukuza sekta ya mawasiliano na kila mtu anufaike na mawasiliano.

Akielezea kuhusu mradi wa kuendeleza maliasili na kukuza utalii mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (REGROW), alisema mradi huo utatumia zaidi ya Sh. milioni 345 kuhakikisha unakuza utalii mikoa hiyo.

■ **Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Francis Godwin (IRINGA)**




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wapili kulia), akitoa maelezo kuhusu bima ya Jahazi kwa Waziri wa Kilimo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (watatu kushoto), wakati wa uzinduzi wa bima hiyo, uliofanyika jijini Mwanza, kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Britam, Raymond Komanga, Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyamagana, Alfred Yonas na Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa NMB, Emmanuel Akonaay (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugai akerwa Bunge kuaibishwa marekebisho ya sheria kila mara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Job Ndugai, amesema anakerwa na uwapo wa marekebisho ya sheria zilizotungwa kwa muda mfupi bungeni kila mara hali aliyosema inaliaibisha Bunge lake.

Ndugai, alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati akifunga mafunzo ya siku mbili kwa mawaziri na manaibu waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

Alisema, moja kati ya mambo yanayomkera bungeni ni uwapo wa mara kwa mara wa marekebisho ya sheria zilizotungwa na Bunge hilo kwa kipindi cha muda mfupi.

"Jambo hili ndugu zangu mawaziri linanikera sana kila tunapokaa vikao vya Bunge Dodoma lazima kuwapo na marekebisho ya sheria ambazo tumezitunga sisi hali hii inaliaabisha sana Bunge.

"Unakuta sheria zingine zimetungwa kwa kipindi cha muda mfupi, lakini zinahitaji marekesho na sisi walewale ndiyo tulio zitunga, zingine kidogo kweli zinahitaji kutokana na kuwa za muda mrefu, lakini hizi zingine siyo sahihi mnawafanya watu wengine hadi wanasema Bunge la Ndugai ni takataka tu," alisema.

Kadhalika, Ndugai alisema sheria ikishatungwa watu wanachofahamu kuwa ni Bunge ndiyo limefanya kazi hiyo siyo serikali wala waziri.

Alisema kutokana na hali hiyo mawaziri wanapaswa kushirikiana kikamilifu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kusiwapo na upungufu ambao utahitaji marekebisho katika kipindi kifupi.

"Sheria ikishatungwa haimtaji waziri wala serikali na watu wanachojua ni Bunge tu ndiyo limeharibu, hivyo tunapaswa kushirikiana kikamilifu kwenye hatua zote ili kuondokana na hali hii," alisema Ndugai.

Aliwakumbusha mawaziri hao kuwa Dodoma ndiyo makao makuu ya serikali na shughuli zote zinapaswa kufanyika hapo na sio vinginevyo.

"Ukienda Marekani kama shughuli ni ya kufanyika Carfonia haitafanyika katika mji mwingine, lakini ukienda Kenya shughuli ya kufanyika Nairobi haitafanyika Kisumu hivyo lazima tutekeleze hili tusiwafanye hadi mabalozi waone kuwa kuhamia Dodoma sio 'issue'," alisisitiza Ndugai.

Vilevile, aliwataka viongozi hao kupendana na kufanya kazi kwa kushirikiana kwa kuwa hivi sasa wapo baadhi yao ambao wanachukiana.

"Tunafahamu kuna baadhi yenu waziri na naibu wake hawapatani lazima tufanye kazi kwa ushirikiano kwani mwisho wa siku serikali yetu ni moja na huwezi jua kesho itakuwaje kama mnakumbuka Sumaye alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu, lakini hakuwahi kuwa hata waziri pia Majaliwa alichaguliwa kuwa waziri mkuu, lakini hajawahi kuwa waziri hivyo naibu waziri wa leo anaweza kuwa bosi wako kesho," alisema Ndugai.

Hata hivyo, aliishauri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kuona ni namna gani inaweza kuweka utaratibu wa kuwapatia mikataba ya malengo yanayofikiwa watumishi wa umma ili kila anayeshindwa kutimiza akitumbuliwa asiwe na sababu ya kulalamika.

"Kupitia mfumo huu kuna jirani yetu nadhani mnamfahamu kafanikiwa sana kwa sababu ya kutumia mfumo huu wa 'Performance Index' hii hata awe rafiki yako lazima ataondoka tu," alisisitiza Ndugai.

## HABARI KITAIFA



Wasafiri wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi za kusini mwa Tanzania jana, walikwama kwa muda katika barabara ya Mlima Kitonga Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa baada ya malori mawili kuharibika kwenye mlima huo, majira ya saa 11 alfajiri hadi saa 2.30 asubuhi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kaburi la mwenye ualbino lafukuliwa, waondoka na viungo

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi mkoani Tanga linawashikilia watu watatu wa familia moja kwa madai ya kufukua mwili wa kijana mwenye ualbino, Heri Kijangwa (45) na kutoweka na jeneza pamoja na mabaki ya mwili wake.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na majina ya watu hao yamehifadhiwa kwa sasa.

"Tunaendelea na uchunguzi kubaini kama kutakuwa na watu wengine wameshiriki, tunataka kujua sababu za kufukua mwili huo na tunataka kujua mabaki ya mwili huo wamepeleka wapi," alisema. Mwishoni mwa wiki, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Under the Same Sun nchini Canada, Peter Ash, alitoa taarifa kwa umma kulaani tukio hilo na kueleza kuwa Heri alifariki Julai 4, mwaka huu kutokana na saratani ya ngozi na mwili wake ulizikwa Julai 7, Kijiji cha Tandwa, wilayani Lushoto, mkoani Tanga.

Ilifafanua kuwa Oktoba 26, mwaka huu, familia ilikuta kaburi limefukuliwa na watu wasiojulikana wakachukua jeneza pamoja na mabaki ya mwili wake.

"Eneo la kaburi hatujakuta jeneza wala mabaki ya mwili wake. Tunalaani kwa nguvu zote tukio hili tunaiomba serikali kufanya uchunguzi na kuchukua hatua madhubuti dhidi ya uhalifu huu nchini," alisema na kuongeza;

"Pia tunaiomba Serikali ya Tanzania kuongeza jitihada za kudhibiti saratani ya ngozi kwa kundi hili. Heri alikuwa ni mnufaika wa programu zetu za elimu, tunasikitika sana kwa unyama huu," alisema. Ash alisema Under The same Sun walimsomesha kijana huyo na kabla ya mauti alikuwa anachukua Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Muhimbili, akiwa amemaliza shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kimataifa na Teknolojia mwaka 2015.

# Majaliwa aagiza nyumba chakavu kukarabatiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza kufanyiwa ukarabati wa nyumba chakavu za wizara na taasisi mbalimbali likiwamo Shirika la Nyumba nchini (NHC) ili ziwe bora ikishindwa kufanya hivyo waziuze kwa wananchi ili zitunzwe.

Vile vile, amewatwisha mzigo wabunge kushughulikia suala la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambayo inasababisha nyumba zinazojengwa na NHC kuuzwa kwa gharama kubwa.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipokuwa akiweka jiwe la msingi la Mradi wa Nyumba 1,000 Dodoma, zinazojengwa na NHC katika Kata ya Iyumbu na Wilaya ya Chamwino.

"Wizara au taasisi mbalimbali ziweke mipango ya kukarabati na kuboresha nyumba za watumishi zinazochakaa, Shirika la Nyumba mna nyumba nyingi sana nchini, hapa Dodoma mbali ya hizi 1,000 zinazojengwa zipo zile za zamani, lakini sio NHC peke yake na TBA (Wakala wa Majengo) mna nyumba nyingi sana, nyumba nyingi zimechakaa."

"Nitoe wito kwenu nendeni mkarabati hizo nyumba ziwe kwenye ubora, mmeshindwa kuzitunza ziuze watu waweze kuzitunza nyumba hizo ili mbaki na chache ambazo mtakuwa na uwezo wa kuzisimamia," alisema.

Alihimiza shirika hilo kuongeza ubunifu zaidi na ubora wa viwango vya nyumba hizo ili ziwe vivutio.

"Nitoe wito kwa taasisi zote zinazojihusisha na ujenzi wa nyumba zihamasishe na kuweka mazingira wezeshi ili wananchi wa maeneo yote nchini wapate makazi kupitia miradi wanayojenga," alisema.

Aliagiza taasisi hizo zinazojenga nyumba za watumishi na majengo ya umma kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu.

"Katika karakana za utengenezaji samani ziboreshwe kimtaji na teknolojia ili kupunguza gharama za uagizaji wa samani nje ya nchi, hapa nimeona mna karakana yenu ya kutengeneza milango na madirisha kwa kuwa nyie mmeamua kuwa na karakana yenu, imarisheni lakini kwa wale wanaotegemea kununua kwenye maduka wakianzisha karakana zao wanarahisisha utendaji na ubora zaidi," alisema.

Alisisitiza miradi ya ujenzi wa ofisi na makazi wigo wake uongezwe nchi nzima na kila idara ijiridhishe kwa kuwa na majengo ya kutolea huduma na NHC ina uwezo wa kujenga.

Majaliwa alisema mradi huo umewezesha kufikia malengo ya serikali ya kutoa ajira kwa Watanzania ambazo 800 zimezalishwa na kuongeza kipato kwa wananchi na kuwataka kuendelea kuchangamkia fursa za ujenzi wa majengo zinazoendelea kwenye maeneo yao.

Naye Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema nyumba zilizopo Iyumbu zinauzwa na zilizopo Chamwino zinapangishwa na haitakubalika mtu mmoja kununua nyumba zote 300 halafu awe shirika la kupangisha wengine.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa NHC, Dk. Sophia Kongela, alisema ili kupunguza uhaba mkubwa wa nyumba bora nchini, Bodi imejikita kuhakikisha shirika linaongeza uwezo wake wa kifedha ili kujenga nyumba za watu wa kipato cha kati na chini huku akisema VAT kwenye uuzaji wa nyumba unaongeza gharama.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulidi Banyani, alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 71 hadi kukamilika na awamu ya kwanza ina nyumba 404 na itagharimu Sh. bilioni 21.4 na hadi kufikia Desemba, mwaka huu, zitakuwa zinakalika.

# CRDB yapata faida bil. 238/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetangaza ongezeko la asilimia 39.9 ya faida kabla ya kodi kufikia Sh. bilioni 238, ikilinganishwa na Sh. bilioni 170 iliyopatikana robo ya tatu ya mwaka 2020.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa mwishoni mwa wiki, faida baada ya kodi iliongezeka kwa asilimia 39.2 hadi Sh. bilioni 168 kutoka Sh. bilioni 120 iliyorekodiwa mwaka uliopita.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa hali hiyo imesababisha mapato yatokanayo na uwekezaji wa wanahisa kukua kwa asilimia 29.3 ikilinganishwa na asilimia 20.9 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Akizungumzia matokeo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema: "Kwa mara nyingine tena, CRDB imeonyesha uthabiti katika kutekeleza ahadi yake kwa wanahisa, wateja, na jamii, ikidhihirishwa na matokeo mazuri iliyopata katika robo ya tatu ya mwaka."

Alisema CRDB inalenga katika kuendeleza ufanisi huku ikidumisha udhibiti thabiti, ikiwa na uhakika wa kufikia malengo iliyojiwekea katika mkakati wa biashara kwa mwaka huu.

"Mapato halisi ya riba yaliongezeka kwa asilimia 11.1 hadi Sh. bilioni 570 katika kipindi cha miezi tisa, hivyo kuakisi uboreshaji wa uchumi wa nchi wakati serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kukabiliana na ugonjwa wa corona," alisema Nsekela na kuongeza:

"Vile vile, mapato yetu yasiyo ya riba yaliongezeka kwa asilimia 12.1 kufikia Sh. bilioni 229 yakichangiwa zaidi na mkazo tuliouweka katika huduma za kidijitali".

Kuhusu matarajio ya kipindi cha mwaka kilichosalia, Nsekela alisema: "Kwa kuangalia mbele, tuko tayari kwa ukuaji mkubwa wa mapato kufikia mwishoni mwa mwaka huu. Ukuaji unaochochewa na huduma zetu za kifedha za kidijitali, mizania thabiti na ufanisi wa kiutendaji".

Ofisa Mkuu wa Fedha wa CRDB, Fredrick Nshekanabo, alisema uwekezaji wa wanahisa uliongezeka kwa asilimia 14.7 kufikia Sh. trilioni 1.1 kutoka Sh. bilioni 974 mwaka 2020, umeifanya benki kuwa na uwezo mkubwa kimtaji.


**KUPOTEA KWA CHETI**



116547102

**ROMWALD PAUL BASHEREKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0115/0110** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya KAHORORO mwaka 1996,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KW/RB/4921/2021**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration
Cause no.162 of 2021
In the matter of the estate of the late EDNA STEPHEN KIMAMBO of CHIDACHI within Dodoma City
And
In the matter of application for letters of administration by ANDREW STEPHEN KIMAMBO AND HAIKA STEVEN KIMAMBO
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before 17/11/2021
Dated at Dodoma this 27/10/2021.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA,LILILOPO BUKOBA

MAOMBI MADOGO NA235/2021

1. ALISON MUTEMBEI
2. FIDELIS KAIZA — WENYE TUZO
3. GOZBERTHA EVARISTA

DHIDI YA

1. METHOD RUTECHURA
2. GODWIN MUTAZAMBA — WASHINDWA HUKUMU
3. TUMAINI MUTAZANGA

KWA: METHOD RUTECHURA
GODWIN MUTAZAMBA
TUMAINI MUTAZAMBA

(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na 235/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 13.12.2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza,R.Mtei saa 2.00 asubuhi.
Hivyo,Mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 12.10.2021

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

HABARI KITAIFA

# Mnada wa korosho wasitishwa kukosekana kampuni za ununuzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

CHAMA Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao, mkoani hapa, kimesitisha kwa muda uuzaji wa korosho kwa njia ya mnada kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wake zikiwamo mwenendo usioridhisha na uhaba wa kampuni zinazojitokeza kununua zao hilo nchini.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Ismaili Nalinga, alisema hayo jana alipozungumza na wakulima wa Kata ya Mtua, Halmashauri ya Mtama.

Nalinga alisema kutokana na mienendo isiyoridhisha ya minada tangu ilipofunguliwa Oktoba mosi, mwaka huu, kunakochangiwa na idadi ndogo ya wafanyabiashara wanaojitokeza kununua zao hilo kupungua na kusababisha bei ya ununuzi kuendelea kushuka kila mnada unapofanyika.

Alisema kampuni 32 zilijiandikisha kununua korosho kupitia Chama cha Lindi Mwambao, lakini zinazojitokeza kufanya ni chini ya hizo, ambazo hata hivyo bei wanazofikia ni ndogo ikilinganishwa na gharama kubwa wanazotumia wakulima katika uzalishaji.

"Hapa leo tumekuja kuwaambieni kuwa mnada hautafanyika hadi Jumamosi ya wiki ijayo," alisema Nalinga.

Pia, alisema kati ya kampuni 32 zinazojitokeza kununua zao hilo ni 10 hadi 16, huku zikipunguza bei kila mnada inapofanyika na kusababisha malalamiko kutoka kwa wakulima.

Aliwaomba wakulima kuendelea kuwa wavumilivu, wakati uongozi wa chama hicho ukiendelea kuwasiliana na serikali ikiangalia ufumbuzi wa tatizo hilo.

Rashidi Mwigero, Hamisi Mikumba na Mwanabibi Yusufu, wakulima wa kata hiyo, wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hizi, waliiomba serikali kuwaangalia mateso wanayoyapata katika uzalishaji wa zao husika.

Walisema kwa misimu isiyopungua miwili sasa zao la korosho limeendelea kushuka bei, hali inayowakatisha wakulima tamaa ya kujikwamua kiuchumi na kujiletea maendeleo ya kujiendeleza kimaisha, ikiwamo kusomesha watoto na kujenga nyumba bora za kuishi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba 100 katika eneo la Chamwino, jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) jana. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo na wanne kushoto ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mwanafunzi bora kitaifa ataka kuwa mpelelezi

**Na Joseph Mwendapole**

MWANAFUNZI bora kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba, Eluleki Haule amesema ndoto yake ni kuwa mpelelezi na kufanyakazi kwenye Idara ya Usalama wa Taifa (TISS).

Akizungumza na gazeti hili mjini Bagamoyo anakosoma masomo ya kujiunga na kidato cha kwanza, Eluleki alisema amekuwa na ndoto hiyo ya kuwa mpelelezi kwa muda mrefu.

Alisema awali ndoto yake ilikuwa kuja kuwa rubani wa ndege kubwa, lakini alibadili ndoto hiyo na kwa sasa hamu yake kubwa ni kufanya kazi ya upelelezi.

"Awali nilikuwa natamani sana kufanyakazi ya urubani na kwa kweli ilikuwa shauku yangu ya muda mrefu, lakini hivi karibuni nimeona nibadili sasa natamani kuwa mpelelezi tu," alisema Eluleki ambaye alisema atasomea masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati.

Akitaja siri ya ufaulu wake, alisema ni kuwa makini darasani, kufanya mapitio ya masomo mara kwa mara, nidhamu na kujituma kwenye masomo na kumcha Mungu wakati wote.

Aliwapongeza walimu wa Shule ya St Anne Marie Academy, kwa kutambua wajibu wao kwa kuwa wamekuwa wakiwapa mitihani na mazoezi mengi hali iliyowaimarisha kitaaluma.

Mama mzazi wa Eluleki, Digna Mlengule, aliliambia gazeti hili kuwa siri ya mtoto wake kuwa namba moja kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka huu ni juhudi zake binafsi na walimu wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Digna alisema Eluleki ni mtoto wa kwanza na wa pekee alikuwa na bidiii ya masomo na hakuwa anahitaji kusukumwa kujisomea wakati wote.

Alisema ni mtu mtulivu, anayejitambua na kufanya mambo yake kwa mpangilio bila kushinikizwi kutimiza wajibu wake kwenye masomo.

"Kwenye suala la masomo hakunisumbua hata kidogo nakumbuka wakati anaanza pre unit tu hapo St Anne Marie ndipo alikuwa anasumbua ila kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba amekuwa mtu ambaye anajua afanye nini bila kusukumwa," alisema.

"Nawashukuru sana walimu maana amesoma pale miaka yote 10 kuanzia chekechea, wamenipa faraja kubwa sana nawapongeza walimu kwa jitihada zao," alisema.

Kuhusu kazi anayotaka kufanya baada ya masomo yake, Digna alisema mara kadhaa amewahi kumsikia Eluleki akisema kuwa anataka kufanya kazi ya kurusha ndege au kuwa mpelelezi kwenye idara nyeti.

Digna alisema kwa sasa Eluleki anasoma masomo ya kuingia kidato cha kwanza na atajadiliana na baba yake ili waone kama aendelee kwenye shule hiyo au wampeleke shule nyingine.

# Zitto ashauri mapato tozo miamala kutangazwa

**Na Gwamaka Alipipi**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema kuna haja kwa serikali kurejea utaratibu wa kutangaza makusanyo ya mapato kutoka kwenye tozo za miamala ya simu kila mwishoni mwa mwezi ikionyesha namna zilivyotumika.

Amesema kwa kufanya hivyo kutawasaidia wananchi kufuatilia na kufahamu matumizi hayo katika ngazi ya vijiji na mitaa.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akihutubia wanachama wa ACT-Wazalendo katika mkutano wa Halmashauri Kuu wa chama hicho, pamoja na mambo mengine aliwataka wajumbe hao kutokukaa kimya katika kuwatetea wafanyabiashara wadogo ambao wamepewa siku kadhaa kutakiwa kuondoka katika maeneo yao ya biashara.

Mfumo mpya wa tozo za miamala ya simu ulianza kutozwa Julai 15, mwaka huu, baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021/22 na wabunge kwenye Bunge la Bajeti.

Zitto alisema serikali ina jukumu la kuwaeleza wananchi kwa uwazi na mara kwa mara matumizi ya vyanzo vya mapato ikiwamo tozo mpya za miamala ya simu.

Alisema serikali ilipitisha tozo mbalimbali ili kukuza mapato ya serikali, lakini tozo hizo zimekuwa kero kwa wananchi.

Zitto alisema pamoja na kutoa maoni ya kuondolewa kwa tozo hilo, lakini serikali bado imeendelea nazo na kusisitiza umuhimu wake na hata kuelekeza maeneo ambayo tozo hizi zimeelekezwa katika matumizi.

Alishauri katika maeneo ambayo fedha za msaada kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) zinachukua nafasi ya tozo hizo ni vyema ziondolewa ili kupunguza mzigo kwa wananchi.

**UCHUMI ZANZIBAR**

Kuhusu hali ya uchumi wa Zanzibar, Zitto alisema Serikali ya Umoja wa Kitaifa mbali na kuleta hali ya utulivu wa kisiasa kisiwani humo, pia imechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uwekezaji na shughuli za kimaendeleo kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka nchi wahisani.

"Miradi ya mashirika ya kifedha duniani kama vile Benki ya Dunia (WB) ambayo ilikuwa imezuiwa kwa muda mrefu kupelekwa Zanzibar sasa imepelekwa, ikiwamo Mradi wa Umeme Zanzibar wenye thamani ya Sh. bilioni 325 na Mradi wa miundombinu ya miji ya Zanzibar wenye thamani ya Sh. bilioni 340".

Vile vile, alisema katika kipindi cha chini ya mwaka mmoja tangu Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuanza, Zanzibar pia imepata fedha kutoka IMF Sh. bilioni 230 kutoka katika Sh. trilioni 1.3 ambazo zimetolewa kwa Tanzania ili kukabili madhara ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Alifafanua kuwa mgawo wa fedha hizo ni asilimia 17.5 ya fedha zote kutoka IMF, ni mara nne ya kiwango ambacho Zanzibar hupewa kutoka kwenye mikopo na misaada.

"Haijapata kutokea Zanzibar kupata mgawo mkubwa kiasi hiki, hili limewezekana kwa sababu ya uwapo wetu kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema Zitto.

**WAMACHINGA KUHAMISHWA**

Aliwataka wajumbe wa ACT-Wazalendo kuhakikisha wanawasemea wafanyabiashara wadogo kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kwa kuwatetea.

"Ndugu wajumbe, hivi sasa kuna zoezi la kinachoitwa kuwapanga wafanyabiashara wadogo wanaoitwa wamachinga. Ninyi viongozi wa mikoa mna wajibu wa kuwasemea wafanyabiashara wadogo. Mnaalikwa kwenye vikao vya Baraza la Ushauri la mikoa yetu (RCC), wasemeeni watu hawa. Tumieni njia mbalimbali za mawasiliano kusemea watu," alisema.

Kadhalika, aliwataka wajumbe hao kutokuwa walalamikaji bali watoe mapendekezo ya majawabu ya nini kifanyike katika kuwawezesha wafanyabiashara hao kuwa na mazingira bora ya kufanyia shughuli zao.

MAKALA

## MIAKA 25 YA REPOA

# Yaanika ilivyozama kumwibua mwanamke katika uchumi binafsi anakokwamishwa

## ■ Yasisitiza utafiti; mila na desturi shida

**Na Salome Kitomari**

WASOMI wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA), wanasherehekea miaka 25 tangu kuanzishwa, ikisimamia majivuno ya utafiti unaoibua mabadiliko ya sera na sheria za nchi na kanda, wakiwanua wanawake ushiriki fursa sawa kiuchumi.

Utafiti wa REPOA umeibua mbinu za kuendelea kuwainua wanawake kiuchumi, kuongeza idadi yao katika kuamua, mabadiliko kisera na kisheria, mnyororo wa thamani, hata hatima ya kinachopaswa kufanyika nchini na nje.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, anasema utafiti unalenga mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ili kumarisha uchumi, kutatua shida katika sekta za kilimo, viwanda, biashara na ukuaji jumuishi unaoleta mageuzi kimaisha.

Dk. Mmari anaainisha, penye uchumi jumuishi kunapaswa kuwapo mifumo ya utawala bora inayounganisha watu kuamua, mifumo ya kusikiliza na kupata maoni, ikiwa ni rasilimali zinazopatikana zinazotumika kwa lengo lililokusudiwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mmari, kuna utafiti wa usawa wa kijinsia na matokeo yake yanashirikishwa kwenye sera mbalimbali kuhakikisha kunakuwapo usawa kijinsia kwenye mfumo wa maendeleo.

Anasema, jamii zimekuwa zikijengewa uwezo kisheria na kisera ili kuendana na mabadiliko, ingawa kuna wanaoachwa nyuma, hasa wanawake akitaja ndiyo mzizi wa kuwapo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Dk. Mmari anasema REPOA ilitafiti mwaka 2014 na kurudia mwaka 2017, ikabaini mabadiliko ikiwamo katika uamuzi ndani ya kaya kumiliki rasilimali maendeleo.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Mmari anasema walipendekeza kuangaliwa mila, desturi, imani inavyochangia uimarishaji usawa kijinsia au walau kupunguza.

Zimebainika sheria za ndoa, talaka na mirathi za kimila au kidini haziwapi fursa wanawake na ndiyo maana wamependekeza mapitio yake.

"Tuna machapisho na kitabu, vijarida na tumeshiriki kwenye mijadala na tukatoa ushauri kuhakikisha viongozi mbalimbali wanasoma," anasema.

**MTAFITI REPOA**

Mtafiti Mwandamizi, Prof. Paschal Mihyo (pichani), anasema REPOA inalenga kuibua fikra za mabadiliko na njia mpya za maendeleo, pia kuchochea jitihada za vyombo vya serikali, asasi zisizo za serikali na wafadhili wakitathmini sera na kinachopaswa kuboreshwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari

Anatoa mfano wa tathmini ya mradi wa uwezeshaji wanawake na mchango wa serikali kusaidia kaya zinazojiweza, inavyowafikia kinamama, hata walazimika kuangalia undani wa mila na aina ya ndoa iliyoko. "Tulivyoangalia kwenye mazingira ya kijinsia, tofauti ya njia za mke zaidi ya mmoja na wengi ni ndogo sana, kwa kuwa bado wanaume wana sauti kubwa katika kutoa maelekezo ya matumizi ya fedha," anasema.

Pia ana angalizo la maeneo wanayodhibitiwa na wanaume kwenye jamii au familia kama vile wajomba wenye sauti kwenye ardhi na mazao, licha ya mwanamke kuwa mshika fedha.

"Ingawa sheria inasema pale sheria ya mila inapokinzana inafuatwa sheria kuu, lakini kwenye jamii hazifuatwi," anabainisha, akitaka kuelewa wale kwa kina uongezwe.

Mtafiti huyo anasema wanashirikiana na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ikiwamo kutengeneza mitaala ya Chuo cha Bunge Arusha, pia walitengeneza mitaala ya wafanyakazi wa mabunge, wakiweka masuala mtambuka ya jinsia.

"Ukizungumzia EAC isiangaliwe kwa ujumla bali kwa makundi kwamba wanawake, wanaume na vijana wanashiriki kwa kiasi gani, biashara za nchi zaidi ya moja," anafafanua.

**WAKOSOA MCHAKATO SHERIA**

Prof. Mihyo anasema "Tunayachokoza mabunge kujiuliza kwanini sheria na sera nyingi zinazotungwa hazitekelezwi? Ndiyo maana tunaanzisha mafuzo ya kutumia tafiti kuunda na kutengeneza sera na sheria."

Anatoa mfano, Sheria ya Makosa ya Kijinsia ya Mwaka (SOSPA) 1998 na sheria ya kukeketa, imekuwapo muda mrefu, lakini makosa yanaendelea kuwapo.

Mtafiti huyo anashauri kufanyike utafiti kuhoji jamii, ili kujenga fikra shirikishi itekelezeke, akikosoa mikataba na sheria zinazoandaliwa na wataalamu wanaopitisha kirahisi, hata kutofanikiwa.

Pia, anataja ilifaki za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) nchi nyingi zinakwama, akiweka pa mfamo wa kurejea taifa la Rwanda limeonyesha hatua ya iliyopiga kato yao, katika eneio huilo la haki na guvu za kijinsia.

Hapo anakumbusha kutunga sheria au sera, inaposhirikisha jamii na makundi inakuwa na mwelekeo unaokubalika.

"Ukiangalia miswada au mikataba iliyogota ni kwa sababu hawakutumia utafiti na shida kubwa kwenye mabunge watafiti ni wachache.

"Masuala ya jinsia unakuta wabunge wanajua zaidi kuliko wafanyakazi wa bunge ambao wanapaswa kusaidia. Hili ni tatizo," analalamika.

Dk. Mmari anasema kila baada ya miaka mitano huwa wanafanya mapitio kudadisi kilichobadilika na walibaini hilo.

"Jinsia ni eneo maalum tunalifanyia utafiti. Tumetengeneza kaulimbiu katika kila eneo na jinsia ni mojawapo ambalo tumefanya na kutoa kitabu," anaeleza.

Anasema, wamefungua mlango wa kujadaliwa maudhui ya vitabu na machapisho kuhusu masuala hayo walioyaandaa na wanatolea ufafanuzi.

**MNYORORO THAMANI**

Prof. Mihyo anasema wanatafiti maeneo mengi na katika mazao korosho, miwa na kahawa wastani asilimia 90 ni wakulima wadogo, wazalishaji wakuu wakiwa kinamama.

Anataja jambo linaloivuta REPOA kuweka kipaumbele kwa kinamama, kuwashirikisha kwenye hatua zote hadi matumizi ya kipato, ikirejea namna serikali inaweza kuwasaidia wakulima binafsi, waliko kinamama wapate haki.

"Tunaendelea na utafiti kuona namna gani wanawake wanaweza kuimarishwa zaidi, ili mnyororo wa thamani usiwaache nyuma kwa sababu za kisheria, desturi au uwezo wa mtaji," anafafanua.

Prof. Mihyo anasema wamebaini tatizo kwenye mfumo wa mauzo mazao ya biashara, anayehesabiwa ni baba na kwenye chakula yuko mama anayewajibika kuhakikisha chakula kinapatikana nyumbani.

Vivyo hivyo, anasema kwenye mifugo mikubwa inashikiliwa na mwanamume na yenye thamani ndogo kama mbuzi, kanga ni vya mama.

"Kwenye jamii kama ya Maasai, ilikuwa nadra sana kuona wanawake wanashiriki mikutano ya kujadili ng'ombe, ila kwa sasa wanashiriki kwa kiasi kikubwa," anadokeza mageuzi yaliyoko.

"Imetokea hata kwenye uvuvi wanawake walikuwa kazi yao kuandaa samaki, wanaume wanavua. Lakini kwa sasa wanaume wanavua na kuandaa samaki na wanawake wameondolewa kiasi cha wengi kukimbilia mjini," anasimulia picha iliyopo.

**UCHUMI MAJUMBANI**

Mabadiliko yaliyoletwa na Uviko-19, imegundulika watu wengi wameondolewa kazini na katika jamii zisizo na mwamko wa usawa kijinsia, mwanaume akipata shida anarudi nyumbani kuchukua majukumu ya uzalishaji ya mke, hali inayompunguzia uwezo kifedha.

Kwenye zao la mwani linalolimwa na kaya zaidi ya 26,000 nchini asilimia 80 kinamama. REPOA imewapa mafunzo kuboresha tija kwenda kwenye kina kirefu na serikali ijue cha kufanya na kushawishi namna ya kuwekeza.

Anasema, hadi sasa wanaofaidi wachache, huku wazalishaji wengi ni wanawake wanaotaabika na Prof. Mihyo anasisitiza wanaendesha mafunzo kwa wakufunzi wa kinamama ili wajishughulishe na uzalishaji mboga hata kufikia ubora unaohitajika sokoni.

Kwa zao la mpunga, kuna mafunzo ya kuwaandaa wakulima wadogo wakikidhi ubora unaotakiwa, kwa masoko makubwa nje ya mipaka.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kutoiunga mkono Simba CAF ni hujuma kwa nchi kuingiza timu 4 kimataifa

LICHA ya kuingiza timu nne msimu huu kwenye michuano ya kimataifa ngazi ya klabu inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho, hatimaye kwa mara nyingine tena ni kama imesalia timu moja pekee, Simba baada ya ombi la Biashara United kutokupatiwa majibu hadi sasa.

Hii ni baada ya Azam FC iliyokuwa ikiiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho kutupwa nje na Pyramids ya Misri huku Biashara United hadi sasa ikiendelea kuisikilizia CAF.

Biashara United ambayo ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya katika mchezo wa awali Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilishindwa kwenda kwenye mechi ya marudiano ugenini kutokana na changamoto ya vibali vya kutumia anga ya Sudan, Sudan Kusini na Libya, hivyo inasubiri kujua hatima yake kutoka CAF.

Kwa upande wa Ligi ya Mabingwa, Yanga iliyokuwa ikiiwakilisha nchi katika michuano hiyo pamoja na Simba, imetolewa, lakini 'Wekundu wa Msimbazi' hao wenyewe wakaangukia Kombe la Shirikisho.

Yanga ilitolewa raundi ya awali na Rivers United ya Nigeria wakati Simba iliyoanzia raundi ya kwanza kutokana na ubora wake msimu uliopita, imetupwa nje na Jwaneng Galaxy ya Botswana na kuangukia Kombe la Shirikisho.

Kwa mantiki hiyo, hadi sasa matarajio ya Tanzania kutetea kuingiza tena timu nne msimu ujao, yapo kwa Simba pekee kutokana na hatima ya Biashara United kutokueleweka. Hivyo, Simba sasa inapaswa kucheza mechi ya mchujo nyumbani na ugenini na kama ikipata matokeo ya jumla itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Tayari wenye dhamana na michuano hiyo, CAF wameshapanga mechi za mchujo ambapo Simba itaanzia nyumbani dhidi ya Red Arrows ya Zambia Novemba 28 kabla ya timu hizo kurudiana ugenini Desemba 5, mwaka huu.

Jambo la muhimu kwa sasa, ni Simba kujiandaa vema kuelekea mchezo huo ili kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo nyumbani kabla ya kwenda kumaliza kazi ugenini, na ikitambua Watanzania wote tupo nyuma yake katika kupigania tena nafasi hizo nne.


Ikumbukwe hadi sasa tayari Libya imefikia pointi za kuingiza timu nne kwenye michuano ya CAF msimu ujao, hivyo kama Simba ikishindwa kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho na kufanya vizuri kwenye michuano hiyo, ni wazi Tanzania itarudi kwenye timu mbili; moja Kombe la Shirikisho na nyingine Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Hivyo, kinachotakiwa kwa sasa ni Watanzania kwa ujumla kuwa kitu kimoja kwa kuiombea Simba katika maandalizi yake na hadi siku itakapocheza mechi hiyo nyumbani na ugenini, tukitambua kwamba inalipigania taifa, hivyo kutoisapoti ni sawa na kuihujumu nchi katika maendeleo ya soka.

Hiki ni kipindi cha kuweka pembeni itikadi zetu za kiklabu na kuwa kitu kimoja na Nipashe tukiwa kama wadau namba moja wa michezo nchini, tunatambua ili kuwa na matarajio makubwa ya timu zetu kufanya vizuri hatuna budi kupigania kuingiza nne kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Nipashe tunaamini kwa yeyote asiyeipa Simba sapoti katika michuano hiyo kwa sasa, basi ni kutokukubali Tanzania kupata nafasi nne katika michuano hiyo msimu ujao jambo ambalo halina tofauti na kuihujumu nchi kisoka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Huu ndio umuhimu wanamichezo, mashabiki kupata chanjo corona

Na Adam Fungamwango

**MICHEZO** ni moja ya kitu ambacho kinawakutanisha watu wengi kwenye sehemu moja, iwe wachezaji, viongozi, wanachama au mashabiki.

Ni kitu kisichoepukika kwa wanamichezo wasichanganyike. Kwa wachezaji ni lazima wakutane wao kwa wao na kisha kwenda kukutana na timu pinzani. Watacheza kwenye uwanja mmoja, watapigana vikumbo na kunyang'anyana mpira au kusemezana wao kwa wao. Mashabiki watakuwa wamekaa majukwaani pamoja.

Kwa kawaida mashabiki wa michezo yoyote ile hawana tabia ya kutengana, mmoja akae hapa na mwingine kule, haiwezekani. Mashabiki hukaa pamoja, wakiimba, kushangilia, na kupiga stori mbili tatu.

Vyote hivi wanavyofanya ni moja ya vyanzo vinavyoambukiza ugonjwa wa COVID -19, unaosababisha na kirusi kiitwacho corona. Na kwa sababu hakuna kitu chochote kinachoweza kusababisha michezo Isiwe na mkusanyiko, kuna umuhimu mkubwa wa wanamichezo wote kupata chanjo ya ugonjwa huo.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikielimisha kuhusu kila Mtanzania kupata chanjo ili kujikinga na ugonjwa huo ambao umepoteza watu wengi sana, hivyo wanamichezo hawawezi kukwepa kuwa moja ya watu wanaotakiwa kuwa mstari wa mbele kuchanja.

Sekta ya michezo, hususan mpira wa miguu ndiyo unaweza kusema inakutanisha watu wengi zaidi kwa wakati mmoja na sehemu moja kuliko sekta nyingine.

Iwe ofisini, viwandani, sokoni, hawawezi kufikia umati unaoingia kwenye viwanja vya soka, na kwa hapa nchini hususan kwa Simba ikicheza, Yanga ikiwa uwanjani, au timu hizo mbili zinapokutana.

Simba na Yanga zinapomenyana kwa Dar es Salaam, inakadiriwa watu zaidi ya 50,000 kuwa uwanjani kwa wakati mmoja, hivyo kwa idadi hiyo kama kuna baadhi hawakupata chanjo kuna kuwa na hatari kuwa ya kuambukizana, na mechi inapoisha kunazalishwa wagonjwa wapya.

Tuliona mwaka 2000, ambapo ugonjwa huu ulifumuka duniani kwa mara ya kwanza, nchi nyingi za Ulaya zilizuia mashabiki kwenda viwanjani. Hii ilisababisha mechi nyingi kuchezwa bila mashabiki. Kusema kweli dunia ilipooza, na soka pia lilipooza.

Msimu huu tumeona mashabiki wameanza kurudi tena viwanjani, hii ni kwa sababu wenzetu wamepata chanjo. Kwa sasa huwezi kuingia kwenye uwanja wowote wa soka Ulaya kama hujapata chanjo, mamlaka zimeanza kuwaruhusu kwa sababu hawana tena tishio la kuambukiza na kuambukizwa.

Siyo kwamba unapokuwa umepata chajo hupati COVID -19, la hasha. Ila ukiupata hauwezi kukusumbua na kukutesa kama mtu ambaye hajapata chanjo kabisa.

Kuna dhana zimejengeka kwenye mitandao ya kijamii na mitaani kuwa chanjo inasababisha upungufu wa kiume baadaye, au kufa kwa mbegu za uzazi. Wengine wanakwenda mbali zaidi kudai eti wakichanjwa, watageuka 'mazombi', yaani yale 'majitu ya ajabu' yanayoonekana kwenye filamu za kutisha.

Lakini tangu Watanzania waanze kuchanja hajawahi kuonekana mtu wa aina hiyo na wala hakuna mtu mwenye ushahidi wa mtu ambaye amegeuka 'zombi'.

Kwa wanamichezo hii ni fursa ya kwenda kupata chanjo ili kuwa na amani wanapokwenda kushuhudia mechi mbalimbali uwanjani, na hata kupata fursa ya kwenda hata nje ya nchi timu za taifa zinapokwenda kucheza, kwa sababu haziwezi kupokea mtu ambaye hana chanjo.

Tuliona wachezaji wote wa Simba, Yanga na Azam wakichanjwa wiki chache kabla ya kuanza mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Wasingeruhusiwa kusafiri na kucheza mechi hizo bila kupata chanjo. Bado tunawaona wachezaji wa timu hizo wakiendelea kucheza. Wakiwa na afya bora. Hatujasikia au kuona mchezaji yeyote wa timu hiyo kageuka 'zombi'.

Kama wachezaji wa klabu hizi wamechanjwa, kwa nini wanachama na mashabiki wanaogopa? Kuchanja ni kwa ajili ya afya yako, kwani huwezi kujua watu unaokaa nao jukwaani kama wana maambukizo au la. Mimi tayari nimechanja, wewe je?

HABARI KITAIFA

# Shahidi wa nne kesi ya Mbowe kusikilizwa leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi leo inatarajia kuanza kusikiliza ushahidi wa shahidi wa nne katika kesi ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Shahidi huyo anatarajia kutoa ushahidi mbele ya Jaji Joackim Tiganga baada ya shahidi wa tatu Koplo Hafidh Mohammed, kumaliza kutoa ushahidi wake Ijumaa iliyopita.

Shahidi wa kwanza katika kesi hiyo alikuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, ACP Ramadhan Kingai na shahidi wa pili, Msaidizi wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, Justine Kaaya.

Shahidi wa tatu katika sehemu ya ushahidi wake akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, alidai Novemba 25 mwaka 2020 akiwa ofisini alipokea vielelezo kutoka ofisi ya DCI ambayo ni bastola aina ya Ruge yenye namba A5340 ya mwaka 1995, vilivyopelekwa kwake na askari aliyemtaja kuwa Goodluck.

Alidai barua iliyopelekwa ilitaka achunguze bastola na risasi kuona kama ni nzima, alianza kuchunguza kwa kupima silaha kwenye kifaa maalum.

Hafidh alidai bastola na risasi tatu baada ya kufanya uchunguzi alibaini vilikuwa vizima na alipopiga risasi mbili kwenye tangi lenye maji ilikuwa inafanya kazi vizuri.

Alidai alipomaliza aliandaa ripoti, akafunga vielelezo kwenye bahasha na kupeleka Amali na Novemba 27, mwaka 2020, afande Swila kutoka ofisi ya DCI alivifuata vielelezo hivyo.

Shahidi aliomba mahakama ipokee ripoti ya uchunguzi kama kielelezo namba mbili upande wa Jamhuri, mawakili wa utetezi walipotakiwa kusema kama wanapinga au hawapingi, walidai hawana pingamizi.

Mahakama ilipokea kielelezo hicho na kuita P2 akimaanisha kielelezo namba mbili cha upande wa Jamhuri, alitoa bahasha alizotunza bastola, risasi, vichwa vya risasi na maganda yake na kuomba pia vipokelewe na mahakama kama kielelezo katika shauri hilo.

Upande wa utetezi kwa mara nyingine hawakuwa na pingamizi, Mahakama ilipokea vielelezo hivyo ambavyo ni bastola namba A5340 ikapewa P3, risasi moja nzima ikawa P4 na maganda ya risasi mbili alizopiga kwenye maji ikawa P4.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

Upande wa Jamhuri unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin Pius Hillar, Jenitreza Kitali, Abdallah Chavula na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.



Mwanafunzi bora kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba, Eluleki Haule, wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri akiwa amebebwa na wenzake baada ya kutangazwa kuongoza matokeo ya darasa la saba Jumamosi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waajiri wanaotumia fedha za SACCOS waonywa

**Na Somoe Ng'itu**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolph Mkenda, amewaonya wakurugenzi wa taasisi kucha 'kuzimezea mate' fedha za waajiriwa ambazo ziko kwa ajili ya kuendeleza mifuko yao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo wa FOSA APP wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo (SACCOS ya TANESCO), wakati wa mkutano mkuu, ulioendana na uzinduzi wa huduma za mtandao za kibenki wa TANESCO SACCOS 'Fosa Mobile App'.

FOSA APP ni mfumo wa fedha kiganjani ambao utawafanya wanachama wa SACCOS hiyo kufanya miamala kirahisi.

Alisema ushirika ni hiari, mali ya wanachama na wao ndiyo wenye uamuzi wa namna fedha zao zitakavyotumika na si vinginenyo.

"Wapo wakurugenzi wanaozimezea mate pesa za wanachama, wanapowakata wanachama mishahara yao kwa ajili ya akiba, hawazipeleki Saccos kwa wakati huo ni wizi. Kama wanataka kuzitumia, basi wafuate utaratibu au wakope kwa riba kwani ile ni mishahara ya waajiriwa walioamua ikatwe kwa ajili ya kujiwekea akiba kwenye chama chao kama wasingekuwa wanachama, wakurugenzi ni lazima wangewalipa waajiriwa hao mishahara yao yote," alisisitiza.

Aidha, waziri huyo alipongeza TANESCO SACCOS kwa kupata hati safi baada ya kukaguliwa na alitaka ni moja ya SACCOS 253 zilizopata hazi hizo kati ya vyama 1,894 vya nchini.

Naye Meneja Mkuu wa TANESCO SACCOS, Andrea Hilary, alisema changamoto ya fedha za wanachama kucheleweshwa kwenye mfuko ipo baada ya wakurugenzi kuchelewa kulipa mishahara.

"SACCOS zinajiendesha kwa michango ya wanachama, hivyo pesa zisipopelekwa kwa wakati ni changamoto ambayo inaweza kusababisha wanachama kukosa pesa za kukopa," alisema meneja huyo.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Afrika, Somoe Nguhwe, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya SACCOS hiyo, alisema anatamani Tanzania irudi kwenye nguvu ya ushirika kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Kuhusu Fosa Mobile App, Somoe alisema itawapa fursa wanachama kupata taarifa zao moja kwa moja kiganjani, kuomba na kupata mkopo wakiwa popote pale bila kufika eneo ambalo akiba zao zinahifadhiwa.

# Nyang'whale yakombolewa barabara

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KATA zaidi ya 10 wilayani Nyang'whale mkoani Geita zimeanza kunufaika na Sh. bilioni 1.5 zilizotolewa na serikali kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na kusaidia kuokoa maisha yakiwamo ya wajawazito.

Mwenyekiti wa Cchama cha Mapinduzi wilayani humo, Alhaji Adam Mtole, alisema katika taarifa yake ya utekelezaji wa ilani ya chama hicho kwa mwaka 2021 na kuunga mkono hatua ya serkali ya wilaya pamoja na ushauri wa Mbunge wa Jimbo la Nyang'whale, Husein Kasu la kutoa kipaumbele kwa maeneo yaliyokuwa yamegeuka kero kwa wakazi wa jimbo hilo.

Akizungumzia utekelezaji huo kwa mwaka 2021 mbunge huyo alisema zaidi ya kata 10 zimenufaika.

Alisema kilichomsukuma kuridhia kwa fedha hiyo kupelekwa vijijini kujenga barabara za vijijini ni kwa kuzingatia kuwa kwa muda mrefu wananchi wamekua wakiteseka kufikia vituo vya kutolea huduma za afya na kusababisha vifo kwa wajawazito, changamoto ambayo amesema kwa sasa imegeuka hadithi.

Vile vile, alisema mwaka 2021 Jimbo la Nyang'hwale ambalo linaunda Wilaya ya Nyang'hwale, wakazi wake wamenufaika na Shilingi bilioni nne zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kijamii ikiwamo ya sekta ya afya, elimu na barabara.

Aliitaja baadhi ya miradi ya barabara iliyotekelezwa ya vijijini kuwa ni pamoja na ya Kharumwa, Bumanda, Nyugwa, Nyijundu, Nyabulanda na Mwingiro na ujenzi wa daraja liliokuwa limekatika ambalo lilikwamisha mawasiliano na kata zingine katika jimbo hilo.

Baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo, wamekiri kuwa hatua hiyo kuwanufaisha ikilinganishwa na kabla ya fedha hiyo kutolewa kutumika kujengea barabara vijijini.

# 159 wakutwa na tatizo la moyo

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI 159 kati ya 230 mkoani Dodoma, waliofanyiwa vipimo kubaini iwapo wana magonjwa ya moyo, walikutwa na matatizo mbalimbali ikiwamo mishipa ya damu ya moyo kuziba, huku 26 wakipatiwa rufani kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi zaidi na kupatiwa tiba.

Idadi hiyo ni kati ya wakazi 319 wa mkoani Dodoma, waliofanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya moyo baada ya kutembelea banda la Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwenye tamasha la Karibu Dodoma Festival.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Anna Nkinda, tamasha hilo lilifanyika kuanzia Oktoba 25 hadi 29, mwaka huu, viwanja vya Chinangali jijini hapo.

Alibainisha kwamba wakazi hao waliotembelea katika banda la JKCI, walifanyiwa vipimo vya urefu na uzito, pamoja na kiwango cha sukari mwilini, uwiano kati ya urefu na uzito, shinikizo la damu na wengine kupata elimu kuhusu magonjwa ya moyo na lishe bora kwa afya ya moyo. "Waliofanyiwa vipimo vya kuangalia jinsi moyo unavyofanya kazi (ECHO) na mfumo wa umeme wa moyo (ECG) walikuwa 230. Kati ya hawa 230 waliofanyiwa vipimo hivi 159 walikutwa na matatizo mbalimbali ya moyo na hivyo kupewa dawa za kutumia.

"Dawa hizi zilitolewa bila malipo yoyote yale na kampuni ya uagizaji na usambazaji wa dawa za binadamu ya Sun Pharmaceutical Industries Ltd," alisema Anna.

Kadhalika, alibainisha kwamba, baadhi ya waliobainika kuwa na matatizo mbalimbali ya moyo walikwenda kufanyiwa uchunguzi wa kina na kutibiwa katika Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa pamoja na ya Mkoa Dodoma, vile vile, wengine kupewa rufani kufika JKCI, Dar es Salaam.

"Matatizo waliyokutwa nayo wagonjwa waliopewa rufani kutibiwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, ni kuziba kwa mishipa ya damu ya moyo hawa walikuwa watano, umeme wa moyo kupita katika njia ya ziada tofauti na ile ya kawaida alikuwa mmoja.

"Mwingine, mshipa mkubwa wa damu wa moyo umetanuka na valvu ya Aorta kurudisha damu nyuma, alikuwa mmoja na mapigo ya moyo yanakwenda haraka kuliko kawaida zaidi ya mapigo 100 kwa dakika moja na inafika wakati anazimia alikuwa mmoja.

Aidha, Anna alifafanua kwamba, mgonjwa mmoja ambaye ni mjamzito moyo wake ulikuwa umetanuka na kuhatarisha maisha yake na mtoto tumboni huku mwingine akiwa na shida ya valvu ya moyo kutokana na bakteria kushambulia valvu za moyo.

"Asilimia kubwa ya wagonjwa tuliowagundua katika upimaji huu, wakiwamo wagonjwa 26 tuliowapa rufani hawakuwa wanafahamu kuwa na matatizo ya moyo.

"Taasisi inatoa wito kwa wananchi kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara pia kujitokeza kwa wingi kupima magonjwa ya moyo wakati tunapotoa huduma mbalimbali za upimaji kwa wananchi."




Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Dodoma, Amosi Mubusi (kushoto), akimkabidhi kadi ya pikipiki ya magurudumu matatu Charles Mkwizu (katikati), baada ya kushinda kupitia kampeni ya Bonge la Mpango 2tumerudi Tena, jijini Dodoma jana, kulia ni Ofisa Huduma kwa Wateja, Neema Kazovio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maonyesho wanasayansi chipukizi kufika wilayani

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amesema serikali ina mpango wa kufikisha wilayani maonyesho ya wanasayansi chipukuzi (YST), ili kuhakikisha kila shule na mwanafunzi anashiriki katika maonyesho hayo.

Profesa Ndalichako alitoa kauli hiyo wakati wa hafla ya kutangaza washindi na kutoa zawadi kwa wanasayansi chipukizi waliofanya vizuri.

Alisema tangu kuanzishwa kwa maonyesho hayo mwaka 2011 ambayo yanatoa fursa kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini kuonyesha kazi zao za kisayansi walizobuni, kumekuwa na mafanikio na hamasa kubwa kupenda msomo ya sayansi.

"Kwa miaka yote 11, kazi ya YST imejikita kutoa hamasa kwa wanafunzi kujikita katika masomo ya sayansi, na mpaka sasa mambo ambayo wanafunzi hawa wanayafanya ni makubwa sana ambayo hayaendani na umri wao na viwango vyao vya elimu, tumeona matunda yake na wametuletea heshima kubwa sana, ninawapongeza," alisema.

Profesa Ndalichako alisema kwa mwaka huu maonyesho hayo yamefanyika katika mikoa 24 tofauti na ilivyokuwa ikifanyika Dar es Salaam pekee na kwamba hayo ni mafanikio makubwa.

"Kwa mara ya kwanza, YST imepata mafanikio makubwa kwa kuendesha maonyesho hayo katika mikoa 24 na kila mkoa umeshirikisha shule zisizopungua 12 na nyingine zaidi ya hizo na kitendo cha kuamua kufanya maonyesho hayo kila mkoa imepanda mbegu, na nina imani kwamba itaota na kustawi na baada ya muda mchache tutaona shule nyingi zaidi zikishiriki."

Alitoa wito kwa wanafunzi wa shule hizo za sekondari kushiriki kwa wingi katika maonyesho hayo mwakani na kupongeza juhudi zinazofanywa na wanaofanikisha maonyesho hayo kila mwaka wakiwamo waratibu kutoka YST, Karimjee Jivanjee Foundation (KLF), Taasisi ya Karimjee Jivanjee Foundation pamoja na Shell Tanzania.

"Teknolojia inabadilika, lazima tuwe na wabunifu ambao kila wakati watakuwa ni chachu ya kuangalia duania inakwenda wapi," alisema Profesa Ndalichako.

Kwa upande wake Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema mikoa ambayo maonyesho hayo yamefanyika mwaka huu, kumekuwa na mwitikio mkubwa na kwamba shule za sekondari 248 na wanafunzi 1158 walishiriki.

Katika maonyesho hayo mwaka huu wanafunzi walioibuka kuwa washindi wa jumla ni Fadhili Shabani na Shufaa Omari kutoka Shule ya Sekondari ya Dk. Salmin Amour iliyopo mkoani Singida.

# Mbaroni kwa kumwingilia mbuzi

**Na Restuta Damian,** KAGERA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia, Emmanuel Zakaria (38), mkazi wa Kata ya Lusahunga, wilayani Biharamulo kwa tuhuma za kumwingilia kimaumbile mtoto wa mbuzi.

Kamanda wa Polisi mkoani mkoani Kagera, Awadhi Juma, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Oktoba 24, mwaka huu wilayani humo.

Alisema mtuhumiwa alipita sehemu na kukuta mbuzi huyo akiwa amefungwa kamba na kuamua kumfungua na kumhamisha kwenda vichakani kisha kuanza kumwingilia.

Aliongeza kuwa wakati akiendelea na kitendo hicho, alipita mwanamke jirani na kumwona ambaye alitoa taarifa kwa wananchi na kumkamata.

"Wakati anahojiwa katika kituo cha polisi wilayani Biharamulo, kijana huyo alidai kuwa alikuwa hapati ushirikiano kwa binadamu kipindi mwili wake ukihitaji," alisema Juma.

Alisema mtuhumiwa anashikiliwa na polisi na baadaye atapimwa akili zake kubaini kama yupo timamu ama ana upungufu.

Wakati huo huo, polisi wanamshikilia mkazi wa mtaa wa Omkigusha katika kata ya Bilele Manispaa ya Bukoba, Anicetha Johanes (24), kwa kukutwa na vifaa tiba vya serikali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 122 pamoja na vifaa vya umeme vya Shilingi milioni nne vya Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Kamanda Juma alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Oktoba 17, mwaka huu majira ya 9:00 alasiri.

Alisema baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa lilifika katika nyumba ya mtuhumiwa na kufanya ukaguzi na kukuta vifaa hivyo.

"Huyu mtuhumiwa anajishughulisha na kuuza vyuma chakavu, lakini kwenye upekuzi tulikuta akiwa na vifaa vya wizi.

Aidha, alisema baada ya kumkuta na vifaa tiba aliwahusisha wataalamu wa idara ya afya ya mkoa huo ambao walivitambua.

# TMDA yataka wataalamu afya kuripoti maudhi chanjo Uviko

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imewasihi wataalamu wa afya na wananchi kutoa taarifa kuhusu madhara/ maudhui yatokanayo na matumizi ya bidhaa tiba ikiwamo chanjo ya Uviko-19, ili zitumike kufanya maamuzi yatakayolinda afya ya jamii.

Kwa mujibu wa TMDA, takwimu zinaonyesha kuwa inapokea taarifa chache ikiwa ni wastani wa ripoti 6,000 hadi 8,000 kwa mwaka, na mwamko wa wataalamu wa afya na jamii katika kutoa taarifa ya madhara ya bidhaa tiba bado ni mdogo; pia taarifa hazina ubora na kukosa baadhi ya taarifa muhimu.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dk. Yonah Mwalwisi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Adam Fimbo, wakati wa uzinduzi wa Kamati ya kitaalamu ya usalama wa dawa, chanjo na bidhaa tiba (VTC), uliofanyika Kibaha-Pwani mwishoni mwa wiki, ukiambatana na mafunzo ya siku tatu na kikao kwa wanachama.

"Kiasi cha taarifa zinazotufikia ni kidogo ukilinganisha na idadi inayopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ya kukusanya angalau ripoti 200 kwa wakazi milioni moja kwa mwaka.

Hivyo kwa idadi ya watu milioni 60 walioko katika nchi yetu, inatakiwa tuwe tunakusanya ripoti 12,000 kila mwaka ili kutoa uthibitisho wa kisayansi juu ya usalama wa bidhaa tiba na kuchukua hatua stahiki," alisema.

Dk. Mwalwisi ameeleza kuwa upatikanaji wa taarifa za kina kuhusu madhara na maudhi ya dawa na chanjo husaidia mamlaka kufanya uamuzi ikiwa ni pamoja na kuziondoa bidhaa kwenye soko, kusitisha ama kubadilisha matumizi.

"Ni tegemeo langu kwamba kamati hii mpya ya VTC iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219 yenye wajumbe 16 wakiwamo wataalamu waliobobea katika tasnia ya dawa na vifaa tiba ambao ni maprofesa na madaktari bingwa, itasaidia sana katika kuhakikisha mifumo ya ufuatiliaji usalama wa dawa, chanjo kwenye soko inaimarika zaidi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Mradi wa Programu ya Dawa, Ufundi na Huduma za Dawa (MTaPs) toka Shirika la Kimataifa la USAID, Dk. Edgar Lusaya, alisema wametoa msaada wa kifedha kwa ajili ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya siku tano kwa wajumbe wa kamati ya VTC ili waweze kufanya ufuatiliaji wa taarifa za madhara ya dawa (ADR).

"Kamati hii ina changamoto ya kufanyakazi ya kushauri vya kutosha kuhusu usalama wa dawa na hasa kipindi hiki tunapozungumzia chanjo ya Uviko-19, kule kwenye vituo kuna changamoto za kuripoti haya madhara wanayopata wadau wetu, tuhakikishe tunayashughulikia. USAID imeweza kutoa mwongozo wa jinsi ya ufanyajikazi wa kamati za dawa na vifaa tiba," alisema.

Kwa upande wake Daktari Bingwa wa Watoto kutoka Wizara ya Afya, Furaha Kyesi, alisema taarifa za madhara ya dawa na chanjo kwa watoto ni chache zaidi, na kuna tatizo kubwa watumishi wa afya wanatakiwa kuelimisha wananchi hatua za kuchukua, na wao wawe tayari kutoa taarifa za sehemu husika.

"Kuna tatizo katika uhamasishaji toka kwa watoa huduma za afya na watumiaji wa bidhaa tiba, hakuna taarifa za juu ya kipi sahihi cha kufanya wanapopata madhara baada ya kupata dawa ama chanjo. Iwapo mzazi ataona mtoto amepata madhara ikiwamo kulia sana baada ya saa 48 kupita au anapatwa degedege baada ya chanjo arejee kituo cha afya kutoa taarifa, na kupatiwa msaada," alisisitiza Kyesi.



Meneja Uhusiano wa Kampuni ya simu ya Vodacom Tanzania, Alex Bitekeye, akigawa vipeperushi kampuni hiyo ikitoa mada juu ya huduma na bidhaa zake wakati wa mkutano wa Wiki ya Azaki uliofanyika jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 10 jela kwa kuua bila kukusudia

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imemhukumu Elikana Kalwemela (47), kifungo cha miaka 10 jela kwa kuua mke wake Chausiku Isengula na mpenzi wa mke wake Agustino Sylivester, bila kukusudia kwa kuwachoma kisu na kufariki dunia.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Jaji wa mahakama hiyo, Fredrick Manyanda, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa.

Jaji Manyanda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Akimsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Kisibo, alidai mshtakiwa na marehemu walikuwa mke na mume na Machi 23, 2016 Chausiku alitoka kwenda Kijiji cha Bweya Wilaya ya Geita kuvuna mihogo na alikaa hadi Machi 28, 2016.

Alidai tarehe hiyo Chausiku alitoka nyumbani kwao na kwenda kupata kinywaji na kukutana na Agustino Sylivester (kwa sasa ni marehemu) kama wapenzi.

Alidai mshtakiwa siku hiyo alisafiri kutoka Kijiji cha wa Ruchili Wilaya ya Sengerema na kumfuata mke wake bila kumpa taarifa.

Wakili huyo alidai, baada ya mshtakiwa kufika kijijini alimfuatilia mke wake na kumuona akiwa na Agustino ndipo alipowafuatilia hadi kichakani na kuwakuta wakifanya mapenzi.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa aliwafuata akiwa na kisu na kuanza kuwachoma wote wawili na kufariki dunia papo hapo.

Baada ya kutekeleza mauaji hayo mshtakiwa alichukua nguo zao na kuondoka nazo.

Alidai kuwa wanakijiji waliona tukio hilo na kutoa taarifa polisi ambao walifika na kuchukua miili ya marehemu hao kwa ajili ya uchuguzi.

Alidai chanzo cha kifo cha watu hao ni kuvuja damu nyingi.

Alisema Machi 29, 2016 mshtakiwa huyo alikamatwa na polisi na alipohojiwa kuhusiama na vifo hivyo alikiri kuwaua mke wake na mpenzi wa mke wake.

Wakili huyo aliomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo kwa kitendo alichokifanya kwa kuwa alikuwa na nafasi ya kwenda kutoa taarifa polisi badala ya kujichukulia sheria mkononi.

Mshtakiwa huyo akiongozwa na Wakili wa kujitegemea Laurenti Bugoti, alijitetea kwa kuiomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu ana watoto sita wanaomtegemea, pia ana tatizo la shinikizo la damu na amekaa mahabusu miaka sita.

Jaji Manyanda alitupilia mbali utetezi huo na kusema mshtakiwa ameua watu wawili kwa pamoja kitendo ambacho ni cha kikatili.

## AMREF yakabidhi majengo, visima

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Utafiti wa Dawa Afrika (AMREF) imekabidhi majengo 19 katika vituo vya afya, visima vya maji 10, ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa Uzazi Uzima unaotekelezwa kwenye halmashauri sita mkoani Simiyu.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Bonifasi Marwa, alisema kuboreshwa kwa huduma hizo kumeongeza idadi ya wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya afya na kupunguza wanaojifungulia nyumbani kwa kutumia wakunga wa jadi.

"Miradi hii imebadilisha kwa kiasi kikubwa hali ya utoaji wa huduma za afya katika mkoa wetu, wakati huu mradi unaanza mwaka 2017 kinamama waliokuwa wanahudhuria vituo vyetu vya kutolea huduma za afya ilikuwa ni asilimia 68, hivi tunavyoongea zaidi ya asilimia 92 wanajifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya," alifafanua.

"Sababu kubwa ni kwamba mazingira yameboreshwa, kwanza mazingira ya kujifungua hayakuwa rafiki kwa kuwa hayatunzi usiri wa kinamama wanapokwenda kujifungua kwa hiyo imejengwa miundombinu mizuri ambayo mama anavutiwa kwenda kujifungua," alisema Marwa.

Vile vile, alisema mradi huo ulihusisha utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa afya katika vituo vya afya na zahanati huduma za msingi za watoto wachanga, kufadhiliwa kwa masomo kwa baadhi ya watumishi kuhusiana na utabibu wa mionzi na utoaji wa huduma za haraka na kwa ukamilifu wa wajawazito.

Awali, Mkuu wa miradi ya AMREF Afrika inayofadhiliwa na Canada, Dk. Aisa Muya, alisema lengo la miradi hiyo ni kuharakisha huduma za afya kwa jamii ili kutimiza ajenda ya afya kwa wote duniani, kipaumbele kikiwa kufikia maeneo yenye uhitaji mkubwa wa huduma hizo na kuwafikia watu ambao kwa muda mrefu wamekosa huduma bora.

"Yapo maeneo ambayo yanaathirika sana na magonjwa kwa kukosa huduma bora za afya AMREF Afrika inalenga kuwafikia watu hao," alisema Dk. Muya.

Kuhusu mafanikio ya mradi huo katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wake, Dk. Muya alisema umesaidia kuboresha vituo vya afya kukidhi mahitaji yaliyopo ikiwamo mafunzo kwa jamii kutambua huduma wanazohitaji na kwamba walitumia mtandao wa wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii takribani 800 na kuwapa mafunzo ya kupeleka katika jamii zao.

## Mkuranga yapongezwa kutambua mchango wa Rais

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Mwanahasha Tumbo, amewapongeza madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa kuutambua mchango wa Rais Samia Suluhu, katika sekta ya elimu.

Pia Rais Samia aliwaletea Wilaya ya Mkuranga zaidi ya Shilingi bilioni tatu za Mpango wa Maendeleo ya Taifa na mapambano dhidi ya Uviko-19.

Katika kikao cha robo ya kwanza cha madiwani wa Halmashauri ya Mkuranga, Katibu Tawala huyo aliwapongeza madiwani kwa kutoa hoja zinazolenga utatuzi wa changamoto zinazoathiri wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ally, alisema wanatekeleza maagizo ya TAMISEMI kwa kuunda kamati kuanzia ngazi ya halmashauri, tarafa hadi kata ili kuhakikisha ubora wa miradi unalingana na pesa.

Ofisa Mipango wa Mkuranga, Kaungwa Aman, alisema tayari wamepokea Shilingi bilioni tatu na kuzielekeza moja kwa moja katika maeneo ya miradi.

Pia kikao hicho kilijadili hoja iliyowasilishwa na Diwani wa Kata ya Magawa, Juma Abeid, aliyezungumzia changamoto za uvamizi wa mifugo kwenye mashamba yenye mazao, migogoro unatishia mauaji ya wananchi.

Diwani wa Kata ya Mbezi Mkuranga, Selungwi Rashidi, kwa upande wake alisema kuna hujuma zinafanywa kwenye minada ya korosho.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Mwantumu Mgonja alisema kuwa, ataitisha kikao cha wadau wa korosho ili kuhakikisha zao la korosho linaleta tija kwa wakulima, halmashauri na Serikali Kuu.

# Madhara rangi madini risasi yabainishwa

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la AGENDA, limesema kuwa ni muhimu jamii ikaongeza tahadhari ya kukabiliana na madhara ya madini ya risasi ni makubwa na ya kudumu hasa wa watoto chini ya miaka sita.

Aidha, madini hayo yanaweza kuathiri ukuaji wa ubongo na kusababisha upungufu wa uwezo wa mtoto kuelewa, mabadiliko ya tabia kama upungufu wa kuzingatia jambo na ugumu wa kufikia malengo ya masoko.

Madini ya risasi hupatikana kwenye rangi mbalimbali hasa zinaposuguliwa baada ya kupakwa kwenye nyumba au eneo lolote. Ofisa Programu Mkuu wa AGENDA, Silvani Mng'anya, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu maadhimisho ya wiki ya kimataifa ya kuzuia madhara yatokanayo na madini ya risasi katika rangi yaliyofanyika kuanzia Oktoba 24 hadi 30, mwaka huu.

"Madini haya risasi yanasababisha upungufu wa damu, shinikizo la juu la damu, matatizo ya figo, ini, matatizo ya kinga ya mwili na matatizo katika via vya uzazi," alibainisha.

Naye Ofisa Programu Mwandamizi wa AGENDA, Dorah Swai, alisema Tanzania kupitia Shirika la Viwango (TBS) ilishaweka kiwango cha madini ya risasi katika rangi tangu mwaka 2017 ambacho ni sehemu 90 kwa milioni (90 ppm).

"Hii ina maana kiasi cha madini ya risasi katika rangi zinazoingizwa, zinazozalishwa, zinazosambazwa, zinazouzwa na zinazotumika hapa Tanzania hakitakiwi kuzidi kiwango hicho.

Pia kwa sasa kuna kiwango kimoja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambacho ni sehemu tisini kwa milioni (90ppm)," alisema na kuongeza; "Rangi zinazozalishwa, kuuzwa au kutumika katika nchi ambazo ni wanachama wa jumuiya hiyo yenye nchi sita ni lazima zikidhi kiwango tajwa."

Kwa mujibu wa Swai, Tanzania ni kati ya asilimia 43 ya nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO) zenye udhibiti wa kisheria kwa mujibu wa taarifa ya Agosti 31, mwaka huu, ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 39 mwezi Mei, mwaka 2020. Alisema kinachotakiwa sasa ni wadau kuongeza juhudi na ushirikiano katika kuhakikisha rangi zenye madini ya risasi zinaondolewa kabisa Tanzania kwa kusimamia utekelezaji madhubuti wa hicho kiwango.

Naye, Katibu Mtendaji wa AGENDA, Haji Rehani, alisema uelewa wa jamii ni muhimu ili kuhakikisha walaji wanaepuka kununua na kutumia rangi ambazo hazijakidhi kiwango cha TBS.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Walaji Tanzania (TCAS), Bernard Kihiyo, alisema Watanzania wanatakiwa kukuza ushirikiano katika kuondoa rangi zenye madini ya risasi kwa kuacha kununua ambazo hazijathibitishwa na TBS.

AGENDA imeungana na taasisi nyingine ulimwenguni zikiwamo asasi za kiraia 49 kutoka nchi 36 ambazo ni wanachama wa Mtandao wa Kimataifa wa IPEN (International Pollutants Elimination Network) kuhamasisha wadau kushirikiana zaidi katika suala zima na kudhibiti rangi zenye madini ya risasi.

Wanafanya hivyo kama sehemu ya kuadhimisha wiki ya kimataifa ya kuzuia madhara yatokanayo na madini ya risasi katika rangi, yanayoratibiwa na Muungano wa Kidunia wa Kuondoa Rangi Zenye Madini ya Risasi ambao uko chini ya Sekretarieti jumuishi kati ya Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa na Shirika la Afya Duniani.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni "Kushirikiana kwa pamoja ili kuwa na dunia isiyo na rangi zenye madini ya risasi."




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (watatu kushoto), akimkabidhi Tuzo Mkurugenzi Mtendaji wa CBM Tanzania, Nesia Mahenge, wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa asasi za kiraia kwenye Wiki ya AZAKI iliyomalizika mwishoni mwa wiki, jijini Dodoma. Wapili kulia ni Karibu Mkuu Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, na (wapili kushoto) Rais wa Foundation for Civil Society (FCS), Stigmata Tenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matukio mauaji Geita yadhibitiwa

**Na Mohab Dominick,** GEITA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, amesema matukio ya mauaji yanayohusisha imani za ushirikina, ukataji mapanga, wivu wa mapenzi, migogoro ya urithi na ugomvi wa mashamba yamekuwa historia mkoani mwake kutokana na ushirikiano mzuri wa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Kamanda Mwaibambe alisema jeshi hilo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio ya kihalifu tofauti na miaka ya nyuma yalipokithiri.

Akitoa historia fupi, Kamanda Mwaibambe alisema Mkoa wa Geita ulimegwa kutoka Mkoa wa Mwanza, ambao una shughuli nyingi za kiuchumi kuanzia uvuvi, uchimbaji wa madini ya dhahabu, maliasili za misitu, kilimo pamoja na ufugaji.

Alisema kutokana na hali hiyo changamoto za kiusalama zinakuwapo na kubainisha kuwa mkoa huo una wilaya tano zote zinajihusisha na shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu na sehemu kubwa zina maliasili na uvunaji wa asali ambao jeshi limedhibiti uhalifu kwa kiwango kikubwa.

Alisema udhibiti huo unaanzia ziwani ambako unaendeshwa na uvuvi haramu na mbinu iliyotumika ni kushirikiana na ushirika wa ziwa BMW na ndiyo maana upatikanaji wa samaki ni mkubwa hasa ukanda wa Geita na Mganza.

Kamanda Mwaibambe alisema wanashirikiana na TANAPA kudhibiti uhalifu na kuongeza kuwa eneo lingine ni la uchimbaji wa dhahabu ambako wanashirikiana na maofisa madini wa mikoa ya kimadini Mbogwe na Geita ambako kuna changamoto nyingi hasa wizi wa kaboni.

Kadhalika suala la maadili kuporomoka ni miongoni mwa jamii kuwapo kwa matukio mengi ya mauaji kwa sababu ya imani za kishirikina, wivu wa mapenzi pamoja na mambo ya migogoro ya ardhi likiwamo la urithi.

"Hivi karibuni Wilaya ya Mbogwe, Mkoa wa Geita kuna mwanamume alimuua mke wake chumbani kisha naye akajiua na wakati akitekeleza tukio hilo alikuwa amefunga mlango huku sauti ya redio yao ikiwa juu ili majirani wasisikie kinachoendelea na mambo kama hayo yanasababishwa na ulevi," alisema Kamanda Mwaibambe.

Alitaja visababishi vingine vya mauaji kuwa ni ushirikina na sehemu kubwa kwa sasa ni migogoro ya ardhi na kuwania mali zilizoachwa na marehemu.

Alisema matukio hayo yaliendelea kupungua kwa kasi kubwa kutokana na kila kata kuweka polisi kata na kuongeza kuwa kadiri elimu inavyoendelea kutolewa mambo haya yanapungua zaidi.

Pia, alisema utumikishwaji wa watoto katika maeneo ya machimbo limedhibitiwa.

Aliwaomba wananchi wa mkoa huo kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa ya mtu wanayemtilia shaka ili wawekezaji waliopata fursa ya kuwekeza katika mkoa huo wanufaike na uwekezaji huo.

"Wakata mapanga maarufu tuliwakamata na tumeamua kufanya operesheni ili suala hili la mapanga liwe historia," alisema.

Alisema kuwa kuanzia kipindi cha mwezi Januari hadi Oktoba, mwaka huu ni tukio moja pekee la mauaji ambalo lililodaiwa lilitokana na imani za ushirikina, lakini baada ya uchunguzi walibaini liltokana na migogoro ya ardhi.

NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 1, 2021
Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WALIOPO EPL WENYE MECHI NYINGI ZAIDI UK. 12


Iniesta

# NYOTA WA5 WANAOWEZA KUWA MAKOCHA WAZURI

**LONDON, England**

KWA miaka mingi, tumejifunza kwamba kuwa mwanasoka mzuri ni jambo moja huku kufundisha na kusimamia timu na kufanikiwa ni suala tofauti kabisa.

Soka la kisasa limetuonyesha kuwa kocha mzuri hakuhusiani sana na kuwa mchezaji bora. Kazi hii inahusiana zaidi na kuelewa mchezo na baadhi ya watu ambao huenda hawakuwa wachezaji wa kuvutia machoni wamekuwa makocha wazuri.

Jose Mourinho ni mfano mzuri wa hili. Hata Pep Guardiola hakutarajiwa kufurahia kiwango hiki cha mafanikio katika kazi yake ya ukocha alipochukuwa mikoba pale Barcelona mwaka 2008.

Hivi majuzi, tumeona wachezaji kadhaa wa zamani wakichukuwa nafasi ya ukocha katika klabu tofauti na kufurahia viwango tofauti vya mafanikio.

Hapa tunawaangalia wanasoka watano wa kisasa ambao wanaweza kuwa makocha wazuri sana hapo baadaye, twende sasa...

**#5. Jordan Henderson**

Kiungo wa kati wa Liverpool, Jordan Henderson alitazamwa na mashabiki wa soka kama si mchezaji mzuri. Alithibitisha namna alivyo bora alipoiongoza Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Henderson amekuwa nahodha wa Liverpool tangu kuondoka kwa Steven Gerrard. Waliosema hana kipaji, amewathibitishia utofauti. Pia ameboresha mchezo wake na amekuwa mahiri chini ya kocha Jurgen Klopp.

Henderson ni mchezaji aliyefanikiwa kufika kileleni baada ya kuvuka bahari iliyochafuka na ni kiongozi wa wanaume. Ameweza kukusanya askari wake na kwenda vitani wakati wowote timu inapomtaka. Kiungo huyo ni hodari katika usimamizi na hakuna shaka atafanya vema katika nafasi ya ukocha kwa siku zijazo.

**#4. Sergio Busquets**

Xavi na Andres Iniesta bila shaka ni ushirikiano mkubwa zaidi wa kiungo wa kati katika soka la kisasa. Hata hivyo, sehemu ya sifa kwa hilo inapaswa kutiririka kwa mwanamume ambaye alikuwa akiwaandalia jukwaa. Sergio Busquets, katika kilele cha nguvu zake, alikuwa kiungo bora zaidi katika mchezo huo.

Mwanasoka mahiri ambaye ufahamu wake katikati ya uwanja ulikuwa wa ulimwengu mwingine, Busquets alikuwa sehemu ya timu ya Pep Guardiola ya Barcelona ambayo ilitawala kabisa Ulaya karibu muongo mmoja. Mhispania huyo amecheza na wachezaji wengine bora kabisa katika historia ya mchezo huo.

Njia ya kazi ya Busquets imekuwa sawa na ile ya Guardiola na hakuna sababu kwa nini ashindwe kuwa kocha bora.

**#3. Toni Kroos**

Toni Kroos ni mmoja wa viungo bora wa kisasa. Amefurahia kazi iliyotukuka na amepata sifa ya juu kwa akili yake ya busara na utoaji wa pasi za ajabu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani ni mmoja wa wanasoka mahiri zaidi duniani.

Anashirikiana vema na washambuliaji wake na pia ni mzuri katika kutekeleza majukumu yake ya ulinzi. Kwa kweli, hakuna chochote ambacho Kroos hawezi kufanya kwenye uwanja wa mpira.

Uzoefu wa Kroos katika kiwango cha juu zaidi, ufahamu wake wa mchezo na ustadi wa busara utamwezesha kuwa kocha mzuri atakapoamua kutundika daluga kwenye uchezaji.

**#2. Cristiano Ronaldo**

Kwa kawaida, washambuliaji ni nadra sana kuwa makocha wazuri. Hata hivyo, huwa inatokeo. Kwa mfano, Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akifanya kazi nzuri kule Manchester United. Kama tu mchezaji mwenzake wa zamani, Cristiano Ronaldo pia anaweza kuwa kocha mzuri.

Ronaldo tayari amethibitisha mara kadhaa kuwa yeye ni kiongozi ndani na nje ya uwanja. Ni mtu ambaye amekuwa akijitokeza kila mara na ameweza kuwatia moyo wachezaji wenzake kufanya vivyo hivyo.

Ronaldo pia amecheza chini ya makocha wakubwa wa zama hizi kama Sir Alex Ferguson, Jose Mourinho, Carlo Ancelotti, Zinedine Zidane, Max Allegri, Rafa Benitez na hata Maurizio Sarri. Amejifunza kutoka kwa walio bora na inajulikana kuwa Ronaldo anafanya kazi kwa bidii kuliko mtu yeyote karibu naye.

Kwa hivyo, hakuna shaka kwamba anaweza kuendelea kuwa kocha mzuri katika siku zijazo.

**#1. Andres Iniesta**


Kwa mbinu yake isiyo na dosari na akili ya mchezo, Andres Iniesta mara zote alikuwa imara zaidi ya wengine alipokuwa akicheza katika kilele cha nguvu zake kule Barcelona. Mmoja wa wachezaji bora katika historia ya mchezo huo, Iniesta anaweza kuzipitia timu zote kwa uwezo wake wa kucheza chenga na pia kuimarisha ulinzi kwa kupiga pasi moja.

Mhispania huyo, ambaye aliifungia Hispania bao la ushindi kwenye fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2010, hajawahi kupata shida kuibuka na kuuruhusu mchezo wake kumzungumziwa. Kwa sasa anachezea Vissel Kobe ya Japan.

Iniesta tayari ameelezea nia yake ya kuwa kocha katika siku zijazo. Uzoefu wake, maarifa, akili na uelewa wake wa mchezo bila shaka utamwezesha kuwa kocha mzuri siku moja.


## ISIKUPITE

LICHA ya kutundika daluga, Petr Cech, bado ndiye kipa anayeshikilia rekodi ya kipa aliyecheza mechi nyingi kwenye Ligi Kuu England bila kuruhusu bao [clean sheet] 202. Lakini ndiye anayeshilikia rekodi ya kumaliza msimu mmoja akiwa na clean sheets 24.



## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOPO EPL WENYE MECHI NYINGI ZAIDI




James Milner

**LONDON, England**

LIGI Kuu England inachukuliwa kama moja ya ligi yenye ushindani zaidi duniani. Hilo limewafanya wachezaji wengi wa kiwango cha kimataifa kupendelea kwenda kucheza huko.

Makala haya inakuchambulia wachezaji kumi waliocheza mechi nyingi zaidi za Ligi Kuu England kwa sasa, shuka nayo...

**#10. Jonny Evans (Leicester City) - 327**

Jonny Evans ni mmoja wa mabeki mahiri wanaopambwa zaidi kwenye Kuu England kwa sasa.

Mshindi huyo mara tatu wa Ligi Kuu amecheza zaidi ya mechi 300 kwenye mashindano hayo, nyingi kati ya hizo (151) akiichezea Manchester United. Sasa akiwa Leicester City tangu msimu wa 2018-19, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa mhimili mkuu wa ulinzi kwa 'Mbweha' hao.

Evans alicheza nafasi kubwa kwa Leicester City katika misimu miwili iliyopita, akikosa mechi kumi pekee, huku timu hiyo ikikosa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. Amecheza mechi mbili pekee msimu huu, kwa sababu ya jeraha alilopata msimu uliopita.

**#9. Shane Long (Southampton) - 332**

Shane Long amecheza zaidi ya mechi 300 za Ligi Kuu akiwa na klabu nne tofauti tangu alipoanza kucheza kwa mara ya kwanza msimu wa 2006-07.

Long, ambaye amekuwa Southampton tangu kuanza kwa msimu wa 2014-15, amekuwa na matokeo ya kawaida katika mashindano hayo. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao 27 pekee ya Ligi Kuu katika misimu yake saba kamili iliyopita. Muda mrefu hajafunga bao kwenye ligi hiyo tangu msimu wa 2019-20.

Hata hivyo, alifunga bao la haraka zaidi la Ligi Kuu kwa Southampton katika historia ya mashindano hayo wakati wa msimu huo. Alifanya hivyo kwa kupachika wavuni ndani ya sekunde 7.69 kwenye mechi dhidi ya Watford.

**#8. David de Gea (Manchester United) - 347**

David de Gea ni mmoja wa magolikipa waliocheza kwa muda mrefu kwenye Ligi Kuu England. Tangu aanze kwa mara ya kwanza kuichezea Manchester United msimu wa 2011-12, raia huyo wa Hispania amecheza takriban mechi 350 za Ligi Kuu.

Mshindi huyo wa Ligi Kuu msimu wa 2012-13, amecheza angalau michezo 26 ya ligi katika kila msimu kumi kamili ya mashindano.

Baada ya hali duni iliyomfanya kupoteza nafasi yake kwa Dean Henderson, De Gea amerejea katika ubora wake msimu huu, akicheza mechi zote nane kabla ya juzi na jana.

**#7. Jordan Henderson (Liverpool) - 368**

Tangu alipocheza mechi yake ya kwanza ya ligi akiwa na Sunderland msimu wa 2008-09, alihamia Liverpool msimu wa majira ya joto wa 2011-12, na amebaki hapo tangu wakati huo. Yeye si mchezaji bora kwenye orodha ya wachezaji nyota wa 'Wekundu' hao, lakini Henderson aliandika historia mwaka 2020 alipokuwa nahodha wa kwanza wa Liverpool kunyanyua taji la Ligi Kuu England baada ya miaka 30.

Henderson ana mabao 31 na asisti 50 kwenye Ligi Kuu, 13 kati ya hayo amefunga akiwa Liverpool. Pia amefunga angalau mara moja katika kila msimu kati ya misimu 12 iliyopita ya Ligi Kuu.

**#6. Ben Forster (Watford) - 368**

Ben Forster amekuwa kwenye Ligi Kuu kwa zaidi ya muongo mmoja. Alipendekezwa kuwa mchezaji muhimu alipowasili Manchester United kipindi cha majira ya joto ya mwaka 2007.

Hata hivyo, baada ya kukosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza, Forster aliamua kuondoka hapo Old Trafford. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alijiunga na Birmingham City msimu wa majira ya joto wa 2010, ambapo alikaa kwa miaka saba kabla ya kusaini Watford mwaka 2018.

**#5. Theo Walcott (Southampton) - 372**

Theo Walcott amecheza zaidi ya mechi 370 kwenye Ligi Kuu akiwa na klabu tatu tofauti. Amecheza mechi nyingi (270) akiwa Arsenal alikokaa kwa misimu 12.

Mara baada ya kuitwa Thierry Henry mpya wakati alipoibukia kwa 'Washikabunduki' hao kwa mara ya kwanza katikati ya miaka ya 2000, Walcott ameshindwa kwa kiasi kikubwa kukidhi hadhi hiyo.

Walcott amefunga mabao matano pekee ya Ligi Kuu katika kampeni zake nne zilizopita za ligi.

**#4. Ashley Young (Aston Villa) - 374**

Baada ya kucheza mechi yake ya kwanza akiwa na Watford msimu wa 2006-07, Young alifanikiwa kwa misimu minne akiwa na Aston Villa. Kisha alihamia Manchester United, ambako alifurahia maisha yenye tija karibu muongo mzima.

Kufuatia kucheza kwa muda mrefu kwenye Serie A, Young amerejea Villa msimu huu wa majira ya joto, na kucheza mechi tano.

Amefikisha mabao 47 na asisti 86 kwenye Ligi Kuu hadi sasa. Alishinda taji lake pekee la Ligi Kuu akiwa na Man United mwaka 2013.

**#3. Aaron Lennon (Burnley) - 392**

Winga huyo amekuwa kwenye Ligi Kuu kwa takriban miongo miwili. Amefanikiwa kucheza takriban mechi 400 kwenye kinyang'anyiro hicho kwa klabu nne tofauti tangu alipoanza kucheza msimu wa 2003-04.

Alikuwa bora zaidi wakati akicheza Tottenham Hotspur, ambapo alifunga mabao 24 na kutoa pasi za mabao 52 katika misimu tisa. Sasa akiwa na Burnley, ambayo alijiunga nayo msimu wa 2017-18, amefunga bao moja pekee katika kampeni zake tano za mwisho za Ligi Kuu.

**#2. Mark Noble (West Ham United) - 405**

Mark Noble ni mmoja wa masalio ya mwisho ya mchezaji wa klabu moja. Tangu acheze kwa mara ya kwanza katika ligi kwa West Ham United msimu wa 2005-06, hivi majuzi alicheza mechi yake ya 400 ya ligi akiwa na 'Wagonga Nyundo' hao wa London.

Noble amejikusanyia mabao 46 na asisti 42 katika klabu hiyo ya London kwenye Ligi Kuu.

Noble hajakaribia kutwaa taji la Ligi Kuu ya England, lakini amekuwa mchezaji thabiti katika mashindano ya West Ham. Ukiondoa kampeni yake ya kwanza na msimu uliopita, Noble amekuwa na mchango angalau wa bao moja katika kampeni 13 mfululizo za Ligi Kuu.

**#1. James Milner (Liverpool) - 568**

James Milner ndiye mchezaji mwenye uzoefu zaidi kwenye Ligi Kuu England kwa sasa.

Milner, kama Lennon, alikuwa mmoja wa wachezaji wachanga zaidi kutokea kwenye Ligi Kuu alipocheza mechi yake ya kwanza pale Leeds United msimu wa 2002-03.

Takriban miongo miwili baadaye, amejikusanyia mechi zaidi ya 550 katika Ligi Kuu England akiwa na klabu sita tofauti. Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 35, hivi majuzi alikuwa mmoja wa wachezaji wakongwe zaidi wa Liverpool kutoa pasi ya bao kwenye ligi.

Milner ndiye mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kusaidia bao kwa Liverpool kwenye Ligi Kuu tangu Gary McAllister aliyefanya hivyo Oktoba 2001 (akiwa na umri wa miaka 36 na siku 299 dhidi ya Leicester).

Ingawa umri umeanza kumtupa mkono, anabaki kuwa mchezaji muhimu katika timu hiyo ya kocha, Jurgen Klopp.


Milner amefunga mabao 55 na kutoa asisti 87 kwenye Ligi Kuu, yakiwamo mabao 19 na asisti 26 kwa Liverpool.

## Nukuu

"Kama Simba wanataka ubingwa wasiuze nyota wao, wakikaa kwa pamoja muda mrefu na kuungana bila shaka watachukua ubingwa na kuwa timu tishio hapa Afrika. Wachezaji waliosajiliwa kwa sasa wengi wao bado wanaendelea kukua, hivyo wakizoea na kuungana na wale waliokuwapo bila shaka watakuwa tishio na hilo lipo wazi," **aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes**



"Hakujawa na wakati ambapo tunasherehekea matokeo viwanja vya ugenini. Kwanza kabisa, ni mapema mno, na pili ya yote tunataka kujikita zaidi badala ya wengine. Kinachoendelea kwa wengine ndicho kitakachokutokea; hatufanyi hivi. Kuna safari ndefu, nina furaha sana leo [juzi] kwa uchezaji wetu tukiwa hatuna mpira. Huu ulikuwa ufunguo kwangu kutoka dakika ya kwanza hadi ya mwisho, juhudi na nidhamu**," Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, baada ya ushindi dhidi ya Newcastle ugenini juzi.**



"Nitangulie kusema kuwa Mungu ndiyo kila kitu, siamini kama leo naondoka Simba. Kwangu ilikuwa familia na najua mashabiki wananipenda sana, ikitokea nafasi ya kurudi pasi na shaka niterejea,**" aliyekuwa Kocha wa mazoezi ya viungo Simba, Mtunisia Adel Zrane, baada ya klabu hiyo kutangaza kuachana naye.**



# LIGI KUU BARA HII SASA HAINA CHA NYUMBANI


Straika wa Yanga, Fiston Mayele, mmoja wa wachezaji waliofunga mabao timu yake ikishinda ugenini.

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na ongezeko kubwa la timu kushinda ugenini kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara msimu huu, hii inaonyesha jinsi gani imekuwa ngumu na kila timu ilivyojizatiti kuona inashinda popote pale, iwe nyumbani au ugenini.

Pia inaonyesha jinsi gani waamuzi msimu huu wamekuwa wakichezesha kwa haki, kwani timu iliyojipanga vema kwa mbinu nzuri za makocha, ndiyo inayoshinda.

Hadi makala hii inaandaliwa zilikuwa zimechezwa mechi 32 za Ligi Kuu, mechi za ushindi zikiwa 20 na sare 12. Kati ya mechi 20 za ushindi michezo tisa timu zimepata matokeo ya ugenini kati ya 11.

Katika makala haya, tumekukusanyia mechi ambazo timu zimekwenda kushinda viwanja vya ugenini, au timu zilizopigwa kwenye uwanja wao wa nyumbani.

**#1. Mtibwa Sugar 0-1 Mbeya Kwanza**

Timu ya kwanza kuonja joto ya jiwe kwa kupigwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, ilikuwa ni Mtibwa Sugar. Ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza Septemba 27. Mbeya Kwanza ndiyo timu ya kwanza msimu huu kushinda mechi ugenini kwa bao la William Edgar.

**#2. Kagera Sugar 0-1 Yanga**

Siku mbili baadaye, Septemba 29 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, Yanga ilikwenda ugenini na kutoa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya wenyeji Kagera Sugar. Lilikuwa ni bao la Feisal Salum lililoifanya mechi hiyo kuwa ya pili kwa timu kushinda ugenini.

**#3. Dodoma Jiji 0-1 Simba**

Simba, ilikuwa ni timu ya tatu kushinda ugenini, ikienda kutoa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Oktoba Mosi mwaka huu. Lilikuwa ni bao La Meddie Kagere lililoifanya mechi hiyo kuingia kwenye rekodi ya mgeni kushinda dhidi ya mwenyeji.

**#4. Biashara United 0-1 Ruvu Shooting**

Siku hiyo hiyo ya Oktoba Mosi kwenye Uwanja wa Karume, Musoma, mkoani Mara, Biashara United ilipoteza mechi nyumbani, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting. Mfungaji wa alikuwa ni Rashid Juma, mchezaji wa zamani wa Simba.

**#5. KMC 0-2 Yanga**

Yanga iliingia kwenye rekodi ya kushinda mechi ya pili ugenini, ilipokwenda kuachia kipigo cha mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, Oktoba 19, mwaka huu. KMC, pamoja na kwamba inatoka Kinondoni, lakini ikahesabika kuwa ni mwenyeji kwa sababu waliamua kuipeleka mechi hiyo kwenye uwanja huo, kama wao wa nyumbani. Yalikuwa ni mabao ya Fiston Mayele na Feisal Salum.

**#6. Ruvu Shooting 0-1 Polisi Tanzania**

Muosha huoshwa! Baada ya kushinda ugenini dhidi ya Biashara United, Ruvu Shooting nayo ilipata mbabe wake, nayo ikaja kupigwa bao 1-0 nyumbani kwake, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani dhidi ya Polisi Tanzania. Mechi hiyo ilichezwa Oktoba 24 huku aliyefunga bao hilo pekee akiwa ni Vitalis Mayanga.

**#7. Prisons 0-3 Biashara United**

Prisons ikaingia kwenye rekodi ya kupoteza mechi ugenini kwa mabao mengi, Oktoba 27 mwaka huu. Ikiwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mjini Sumbawanga, ambao ni msimu wa pili, inautumia kama uwanja wa nyumbani, ilikubali kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Biashara United. Ikumbukwe kuwa Biashara United ilishapigwa ugenini na Ruvu Shooting.

Nayo ikapata mnyonge wake kwa kuifunga huko huko kwao, kwa mabao ya Ramadhani Chombo 'Redondo', Denis Nkane na Ambroce Awio.

**#8. KMC 0-1 Kagera Sugar**

KMC, baada ya kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Yanga, ikapoteza tena mechi nyumbani kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar Ijumaa iliyopita ya Oktoba 29. Safari hii ni kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. Hii ikawa ni mara ya pili kwa KMC kupoteza nyumbani. Kagera Sugar ambayo ilishapoteza dhidi ya Yanga nyumbani, nayo ikapata kibonde wake wa kumpiga nyumbani kwake kwa bao la Meshack Abraham.

**#9. Mtibwa 0-1 Dodoma Jiji**

Kwa mara nyingine tena, Mtibwa Sugar imepigwa nyumbani, dhidi ya Dodoma Jiji kwa bao 1-0 kwenye mechi iliyochezwa Jumamosi. Awali ilifungwa na Mbeya Kwanza. Bao la Dodoma Jiji likiwekwa kambani na Seif Karihe.

**JE, WAJUA?**




KATI ya nchi 12 zilizoingiza timu nne kila moja kwenye michuano ya CAF; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, ni nchi tatu tu ambazo timu zao zote bado zimebaki katika mashindano hayo; Algeria (CR Belouizdad, ES Setif, JS Kabylie na JS Saoura), Misri (Al Ahly, Zamalek, Al Masry na Pyramids) na Afrika Kusini (Mamelodi Sundowns, AmaZulu, Gallants na Olando Pirates)





Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Makole, Askofu Evance Chande, akiwaombea wanafunzi wa kidato cha nne na pili ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani yao inayoanza leo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# AZAKI zashauri taarifa za rasilimali zitinge bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASASI za Kiraia (AZAKI) zimelishauri Bunge kutafuta namna ya kuziingiza bungeni ripoti za ukaguzi zinazofanywa na mashirika binafsi kwa ajili ya kujadiliwa, ili kuokoa fedha ambazo zinapotea katika sekta ya madini, mafuta na gesi nchini.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki wakati wa mjadala ulioratibiwa na Shirika la HakiRasilimali kwenye maadhimisho ya Wiki ya Asasi za kiraia (AZAKI) yaliyofanyika jijini hapa.

Mjadala huo uliendeshwa na Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na washiriki walikuwa ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mstaafu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga.

Katika mjadala huo Kabwe alisema ripoti nyingi ambazo zinatolewa na taasisi mbalimbali binafsi haziwezi kuingia bungeni kwa ajili ya kujadiliwa hali ambayo inachangia kuendelea kupoteza fedha nyingi katika sekta ya uzinduaji.

"Mheshimiwa Hasunga kuna ripoti ya Taasisi ya Uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia (TEITI) imetolewa, lakini inaonekana kwa mujibu wa kanuni za kibunge haiwezi kuingizwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa hakuna namna ambayo inaweza kutumika na bunge ili ripoti hizi ziweze kujadiliwa bungeni," alihoji Kabwe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Rachel Chagonja, alihoji sababu ya taasisi mbalimbali ambazo zinajihusisha na kufanya ripoti za ukaguzi hazijadiliwi bungeni licha ya kuwa zinabaini kuwapo kwa upotevu wa fedha nyingi katika mashirika ya umma.

"Sheria inasema kuwa CAG, hawezi kukagua kampuni ambayo serikali ina hisa chache hivyo bunge halioni kuwa kuna namna inatakiwa kutafutwa ili kampuni zetu za madini ziweze kufanyiwa ukaguzi," alihoji.

Akijibu hoja hizo, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Hasunga alisema kwa mujibu wa kanuni za Bunge, ripoti zote zinazofanywa na mashirika haziingii bungeni kwa ajili ya kujadiliwa.

"Ni kweli ripoti zote zinazofanywa hadi hii ya TEITI ambayo imezinduliwa leo haziingii bungeni kwa ajili ya kujadiliwa, lakini kupitia Mbunge mmoja mmoja anaweza kuzipata na kuzisoma na akaona kitu ambacho anaweza kuja nacho bungeni kwa ajili ya kuwasilisha hoja yake," alisema Hasunga.

Vilevile, Hasunga alisema kutojadiliwa bungeni ripoti hizo ni matakwa ya kisheria, lakini hali hiyo haimzuii mtu moja mmoja kuipata ripoti hiyo na kuijengea hoja akiwa ndani ya bunge.

"Wabunge wamekuwa wakipokea ripoti za wakaguzi wa mashirika binafsi na kupeleka hoja bungeni na hiyo haizuiliwi kwani ni haki na mara nyingi imekuwa ikifanyika hivyo," alisema Hasunga.

Naye Prof. Assad aliishauri serikali kufanya shughuli zote za kimikataba kuwa wazi.

Prof. Assad alisema kuwa inatia shaka kama jambo dogo la vikao vya Bunge kurushwa mubashara limeshindikana na kwamba itawezekanaje mambo mengine makubwa yenye maslahi na taifa.

# Waziri atoa miezi saba utekelezaji miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka watendaji wa sekta ya maji nchini kutekeleza miradi kwa uaminifu ndani ya miezi saba, ili wananchi wa vijijini wapate huduma hiyo kwa haraka.

Aweso aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watendaji hao kuhusu utekelezaji wa miradi 2018 ya maji mijini na vijijini ambayo fedha zake zimetokana na wizara kupata mgawo wa Sh. bilioni 139.4 za mapambano ya Uviko-19 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Alisema miradi hiyo inapaswa kutekeleza kwa uadilifu, ubora, uhalisia wa gharama na kwa wakati ili wananchi waondokane na adha ya maji.

"Fedha tunazo tumeshapewa twendeni tukafanye kazi. Nawapa ushauri wa bure unaweza kukosa Uviko-19 ukapata fedha zake, hizi fedha hazilambwi, tumekutana hapa tunaelekezana ni aibu kubwa Mhandisi unakuja kufukuzwa kizembe eti umechukua fedha kiasi fulani," alisisitiza.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliwataka watendaji hao kwenda kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

"Hata uwe mtendaji mzuri vipi kama huna nidhamu kwa mwenzio unaweza kupoteza maana," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, alisema lengo la kikao hicho ni maelekezo mahususi ya utekelezaji ya miradi hiyo na kusisitiza kuzingatia maelezo waliyopewa.

"Tukasema lazima tuitane wote watekelezaji wa miradi na kuwapa maelekezo na msije mkakosea, sababu ni hatari kubwa kutumia pesa hizi tofauti na maelekezo ambayo mmepatiwa, tumepanga kutekeleza miradi takribani miradi 218," alisema.

# Bilioni 51 zajenga majengo ya kutolea haki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetumia Sh. bilioni 51.45 kujenga majengo sita ya kisasa ya vituo vya kutolea haki ili kupunguza mrundikano wa kesi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Othman Makungu, aliyasema hayo jana kwenye ziara ya watumishi wa mahakama kutoka Zanzibar waliotembelea kituo jumuishi cha utoaji haki kilichopo jijini hapa.

Alisema kupitia ujenzi wa vituo hivyo mrundikano wa kesi utapungua kwenye mahakama kutokana na kuharakisha upatikanaji haki kwa wananchi.

"Sasa hakuna visingizio vya kesi kuchelewa kusomwa kupitia vituo hivi tuna imani kesi zote zitamalizwa kwa haraka na watu kupata haki zao bila upendeleo," alisisitiza. Jaji Makungu aliishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wake pamoja na mahakama kwa kuwajengea majengo hayo ambayo yanakwenda kupunguza mzigo mkubwa wa kazi za utoaji haki kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel alisema; "Suala la mahakama sio Muungano, lakini tunapokuja kwenye suala la haki inatenda haki kwa wote na ujio wa watumishi kutoka Mahakama ya Zanzibar ni moja ya kuonyesha Watanzania na Wazanzibar ni wamoja."

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama Zanzibar, Kai Mbaruk, alisema kwa muda mrefu Mahakama ya Zanzibar inakabiliwa na tatizo la majengo, lakini kwa sasa limetatuliwa.

Alisema wamefanya ziara hiyo kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali hasa kwenye jengo jipya la kituo hicho na kwamba yatawasaidia kuboresha ya kwao ili haki za wananchi zipatikane kwa urahisi.

"Tunashukuru na tunawapongeza kwa kuwa na majengo hayo inaonyesha jinsi gani serikali inavyowajali wananchi wake," alisema Mbaruku.





# Wanawake kipato cha chini kuanzishiwa biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE watano wa kipato cha chini katika Mkoa wa Mbeya wanatarajiwa kunufaika na msaada wa kuanzishiwa biashara na kupatiwa elimu ya utunzaji wa fedha kila mwaka ili kupunguza kiwango cha umaskini kwenye familia hizo.

Fedha hizo zitakuwa zinatolewa na Shule ya Paradise Mission Pre and Primary School iliyopo katika Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya ambayo itakuwa inatenga bajeti ya Sh. 3,000,000 kila mwaka kwa ajili ya kusaidia kundi hilo.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Ndele Mwaselela aliyasema hayo juzi wakati wa Siku ya Wakurugenzi wa Biashara iliyoandaliwa na mtandao wa wajasiriamali ujulikanao NAAZAH Group ambao ndio waanzilishi wa wazo la kuwasaidia wanawake.

Aliwataka wanachama wa NAAZAH Group kumpelekea majina ya wanawake watakaokuwa wamechaguliwa mwezi mmoja kabla ya siku ya uwezeshaji, ili kumpa nafasi ya kuandaa vizuri bajeti kwa kushirikiana na uongozi wa shule.

"Nyie fanyeni mchakato wa kuwapata hao wanawake mkimaliza mnileteeni majina na ninawahakikishia kwamba sitawaingilia kwenye mchakato wenu ila nitatoa fedha, hili ni wazo zuri ambalo naamini litasaidia kuzikomboa hizo familia za wanufaika," alisema Mwaselela.

Aliwapongeza wanachama wa mtandao huo ambao wengi ni wanawake kwa ubunifu wa biashara na akawataka kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha ili biashara zao zikue na wawe miongoni mwa wawekezaji wakubwa ndani na nje ya nchi.

Awali, Mkurugenzi wa NAAZAH Group, Nazarena Myenzi, alisema umoja huo una utaratibu wa kuwawezesha wanawake wasiojiweza kuanzisha biashara kila mwaka na kuwafundisha namna ya kutunza fedha ili ziwasaidie kuendesha maisha yao.

Nazarena ambaye kitaaluma ni Ofisa Ustawi wa Jamii alisema katika shughuli zake amekuwa akikutana na baadhi ya familia za wanawake wenye maisha magumu kutokana na kutokuwa na vitega uchumi na baadhi yao hawana makazi bora.

"Tuna utaratibu wa kuwawezesha wanawake kufungua biashara na kuwapa elimu ya utunzaji sahihi wa fedha na kwa mwaka huu tayari tumeshafanya hilo, lakini pia tunawasaidia wanawake wahitaji angalau wawe na uwezo wa kujikimu na tunatarajia kufanya hilo mwezi Disemba mwaka huu," alisema Myenzi.

Alisema kundi hilo lina utaratibu wa kuwafundisha wanachama kutunza akiba ya fedha na kwamba mwaka jana kuna baadhi ya wanachama walitunza mpaka akiba ya zaidi ya Sh. milioni 25.

Vilevile, alisema wameanzisha vikoba kwa ajili ya kusaidiana kuinuana kiuchumi na kwamba wana utaratibu wa kutembeleana ili kujionea maendeleo ya biashara ya wanachama na kuwasaidia kati ya Sh. 500,000 na 800,000.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Makambili iliyoko Mji wa Tunduma mkoani Songwe, wakinawa mikono hivi karibuni kwenye miundombinu waliyojengewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wake wa SAWA, wanafunzi hao walikuwa wanawa wakati wa uhamasishaji wa usafi wa mazingira uliofanywa na maofisa hao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanajeshi Tanzania, Malawi watembelea vivutio Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MAJESHI ya Tanzania na Malawi Brigedi za mpakani, yameungana kwa pamoja kutembelea vivutio vya utalii mkoani Mbeya, kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji hasa kwenye ulinzi wa mipaka baina ya nchi hizo.

Vikosi vya majeshi hayo vilivyoungana ni brigedi namba 401 yenye makao yake Songea mkoani Ruvuma kwa upande wa Tanzania na Brigedi namba 101 kwa upande wa Malawi na kutembelea Ziwa Ngosi lililoko Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya. Maafande hao ambao walipiga kambi ya pamoja jijini Mbeya walitembelea kivutio hicho kutokana na kuwa miongoni mwa vivutio ambavyo vipo karibu na eneo ilipo kambi yao pamoja na sifa zake. Mmoja wa makamanda wa Brigedi ya Kusini mwa Tanzania, Kanali Chirian Ng'abi alisema waliamua kuwapeleka majirani zao katika kivutio hicho, ili kuwaonyesha utajiri wa Tanzania kwenye mambo ya utalii na kwamba ziwa hilo lina sifa ya kipekee.

Alisema ziwa hilo lipo milimani, halina mto unaoingiza maji wala unaotoa na lina umbo lenye mwonekano wa ramani ya Bara la Afrika na maji yake yanavutia kutokana na kubadilika rangi mara kwa mara.

"Ukija hapa huwezi ukatamani kuondoka, tulipokuwa tunafika maji yalikuwa na rangi ya bluu lakini sasa hivi yameshabadilika na kuwa ya kijani, lakini ukiliangalia linaonekana kuwa na ramani ya Afrika pamoja na visiwa vyake," alibainisha Kanali Ng'abi. Aidha, aliwataka Watanzania kuendelea kufuatilia vivutio vya utalii vilivyomo nchini badala ya kuwaachia wageni kutoka mataifa mengine huku akiwataka wananchi kuacha kuamini imani zinazoenezwa na baadhi ya wapotoshaji.

Brigedi Kamanda wa Brigedi ya Kusini mwa Tanzania, Charles Feruzi, alisema ziara hiyo iliwafundisha vitu vingi ambavyo walikuwa hawavijui kutokana na maelezo ambayo walielezwa na wataalamu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS).

Kwa upande wake Brigedia Kamanda wa Brigedi namba 101 ya Malawi, Godfrey Kumwenda, alilishukuru Jeshi la Tanzania kwa kuwatembeza kwenye kivutio hicho na kwamba hawajawahi kuona kivutio kama hicho.

Alisema nchini Malawi hakuna kuvutio chenye sifa kama Ziwa Ngozi na hivyo baada ya kutembelea walipata kitu cha kwenda kusimulia kwao pamoja na kuwahamasisha Wamalawi kutembelea vivutio.

"Tunawashukuru wenzetu Watanzania, ziara yetu ni ya kuimarisha ujirani na wameamua kututembeza kwenye kivutio hiki cha aina yake, tumefurahi na tunaamini wataendelea kutuonyesha vivutio vingi zaidi," alisema Kamanda Kumwenda.

Awali, kabla ya kutembelea ziwa hilo walishiriki kwenye michezo ya pamoja ambayo ilikuwa ni mashindano ya mpira wa miguu kwa wanaume na mpira wa pete kwa wanawake.

# SACCOS zashauriwa kupunguza riba

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

VYAMA vya kuweka na kukopa (SACCOS) nchini vimeshauriwa kupunguza riba za mikopo ambayo vinatoa kwa wanachama wake, ili kuwavutia watu wengi zaidi kujiunga na vyama hivyo pamoja na kuwapunguzia mzigo wanachama.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Mbeya na Mrajisi Mkuu wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Niege, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 13 wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Usalama wa Raia (URA SACCOS) kinachomilikiwa na Jeshi la Polisi. Alisema vyama hivyo vikipunguza riba vitakuwa tofauti na taasisi zingine za kifedha na hivyo wanachama wengi watakuwa wanakopa fedha kwenye vyama vyao badala ya kukimbilia kwenye taasisi nyingine. Alisema kitendo cha vyama hivyo kuwa na riba kubwa ni sawa na kwamba wanachama wanajinyonya wenyewe na kwamba vyama hivyo haviwezi kuwasaidia kujikwamua na umaskini.

"Nimefurahi kwamba URA SACCOS riba yenu ni asilimia nane, lakini nawaomba muone namna ya kufanya ili ikiwezekana ipungue zaidi, angalau hata ikiwa asilimia saba inakuwa nafuu zaidi, kuna vyama vingine riba ni kubwa zaidi," alisema Dk. Ndiege.

Aidha, aliwapongeza viongozi wa chama hicho kwa usimamizi mzuri unaokifanya kuwa miongoni mwa vyama vinavyoendeshwa kwa weledi zaidi nchini na kwamba ni moja kati ya vyama ambavyo mwaka wa fedha uliopita Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) vilipata hati safi.

Katika hatua nyingine alivishauri vyama vya ushirika kubadili uendeshaji wa vyama hivyo ikiwamo kuanza kuviendesha kwa njia ya TEHAMA ili viendane na mabadiliko ya teknolojia yaliyopo sasa hivi.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya URA SACCOS, Kamishna wa Polisi (CP) Benedict Wakulyamba,alisema pamoja na kwamba chama hicho kimeundwa ndani ya Jeshi la Polisi lakini uendeshaji wake unazingatia misingi ya uendeshaji wa ushirika.

Wakulyamba ambaye ni Kamishna wa Polisi Utawala na Raslimali Watu, alisema chama hicho kinawashirikisha maaskari wa nchi nzima na kwamba katika kila wilaya kuna tawi la chama hicho pamoja na Zanzibar. Alisema licha ya kwamba chama hicho kinafuata maadili ya kijeshi, lakini linapokuja suala la uwakilishi katika uendeshaji wa URA Saccos, demokrasia huchukua mkondo wake bila kujali cheo cha mwanachama ndani ya Jeshi la Polisi.

"Uendeshaji wa chama chetu hasa katika eneo la uwakilishi tunazingatia sana misingi ya demokrasia, na ndio maana humu ndani utasikia kuna askari mwenye cheo cha konstebo ambacho ni cha chini kabisa ndani ya jeshi letu mpaka makamishna wamo," alisema Wakulyamba.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP), David Misiime ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya URA SACCOS alisema chama hicho kimekuwa na mafanikio makubwa ndani ya miaka michache.

Alisema mbali na kupata hati safi mwaka wa fedha uliopita lakini kilipata tuzo ya kuwa moja ya vyama vinavyoendeshwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na serikali.

Mkutano huo wa mwaka uliwashirikisha wajumbe zaidi ya 200 wa wilaya zote nchini ambao kwa mujibu wa Katiba ya URA SACCOS wanachaguliwa na wanachama kwenye maeneo husika na kwamba Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi (IGP) ndiye mlezi wa chama.



# ZIPA kuadhimisha mwaka 1 wa Rais Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), imeandaa ufunguzi na uwekezaji wa mawe ya msingi katika miradi mbalimbali ya uwekezaji Unguja na Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kukaribisha uwekezaji katika sekta tofauti na kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Dk. Mwinyi, kuna maendeleo mbalimbali yamepatikana katika miradi ya uwekezaji.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo tangu Novemba, mwaka jana hadi Oktoba, mwaka huu kuna jumla miradi 73 ya uwekezaji jambo ambalo halijapata kutokea katika miaka iliyopita. "Licha ya changamoto ya maradhi ya corona ambayo yameikumba dunia, lakini miradi 73 tumeipata kwa muda wa mwaka mmoja ambapo katika miaka ya nyuma haijawahi kutokea maana miaka hiyo huwa tuna wastani wa miradi 30 ya uwekezaji," alisema.

Alisema uchumi wa Zanzibar ni wa kisiwa na miradi mingi ya uwekezaji ni uchumi wa masuala ya huduma za utalii, lakini kwa sababu ya sera nzuri ya Rais ya uchumi wa bluu, mamlaka hiyo imeweka kipaumbele katika viwanda, kilimo, utalii na masuala mengine yatakayosaidia kuleta maendeleo ya nchi.


Naye Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Huduma wa Mamlaka hiyo, Shida Makame Kombo, alisema miradi hiyo 73 ina mtaji wa Dola za Kimarekani, milioni 477 na serikali ya Zanzibar itapata fedha hizo kupitia uwekezaji.

Alisema miradi hiyo itatoa ajira 579 na wananchi wazawa ndiyo watapewa kipaumbele.

"Miradi hiyo 73 wawekezaji wake ni raia wa kigeni na wenyeji, lakini mingi yao ni wawekezaji wazawa ambapo hali hiyo inadhihirisha wenyeji walivyokuwa makini katika kupeleka mbele gurudumu la uchumi," alisema Shida. Shughuli ambazo zinatarajiwa kuzinduliwa na kuwekewa jiwe la msingi katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa uongozi wa Dk. Mwinyi ni uwekezaji wa jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Riu huko Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja utakaoanza kesho na mgeni rasmi katika shughuli hiyo ni Rais Mwinyi.

Baada ya shughuli hiyo kutakuwa na uwekaji wa jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa hoteli ya Emerald (Palolo) huko Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja, uwekaji wa jiwe la msingi katika mradi wa nyumba za biashara huko Bweleo Mkoa wa Mjini Magharib Unguja na ufunguzi wa mradi wa nyumba za biashara, Chukwani Mjini Unguja.

Pia Novemba 3, kutakuwa na uwekaji wa jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa Hoteli ya L'oasis, Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja, ikifuatiwa na ufunguzi wa kiwanda cha kutengeneza vipodozi mradi wa Shear Illusion, Maruhubi Mjini Unguja, ufunguzi wa viwanda, Amani Mjini Unguja Novemba 4, na Novemba 5 ni uwekaji wa jiwe la msingi kiwanda cha vinywaji Chamanangwe, Kisiwani Pemba.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Omar Shaban (wa pili kushoto), akiwa pamoja na ujumbe wa Bank of Africa (BOA) ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu mpya, Adam Mihayo (kushoto), ulipotembelea ofisini kwake jana, wengine pichani ni Naibu Mkurugenzi wa BOA, Samir Yassine (kulia) na Mkurugenzi wa Wakala wa Kuendeleza Biashara Ndogo na Kati Zanzibar, Soud Ali. **MPIGAPICHA WETU**

# Marekani kutoa dozi mpya chanjo Uviko-19

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAREKANI inakusudia kutoa dozi mpya ya chanjo ya corona aina ya Pfizer kwa Serikali ya Zanzibar ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kupambana na ugonjwa wa Uviko-19 na kupunguza athari za kiafya kwa wananchi wake.

Hayo yalisemwa juzi na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, Mjini Unguja.

Balozi huyo alisema Marekani imejipanga kujikita kusaidia sekta ya afya kupitia mashirika yake ikiwamo Shirika la Msaada wa Maendeleo la Marekani (USAID) na kuona maradhi yanadhibitiwa ikiwamo yale ya hatari yanayosababisha vifo kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar kupambana na ugonjwa huo ikiwamo kutoa elimu zaidi kwa walengwa, kuona athari za kiafya zinapungua hatua ambayo imesaidia ugonjwa huo kuwa sio tishio kwa afya za wananchi. "Serikali ya Marekani inaahidi kusaidia sekta ya afya kukabiliana na maradhi mbalimbali ambayo ni tishio kwa afya za wananchi, tupo tayari kutoa chanjo zaidi za kujikinga na ugonjwa wa Covid -19 aina ya chanjo ya Pfizer," alisema.

Naye Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii, jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, aliipongeza Marekani kwa misaada yake katika sekta ya afya ikiwamo mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19 ikiwamo kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii. Mazrui alisema misaada inayotolewa na nchi hiyo imeleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Zanzibar ikiwamo mapambano dhidi ya maradhi yasiyoambukiza ambayo hivi sasa yanaongoza kwa kusababisha vifo vingi.

"Serikali ya Zanzibar inaridhishwa kwa kiwango kikubwa misaada inayotolewa na Marekani ambayo imejikita katika sekta mbalimbali ikiwamo afya katika kupambana na maradhi ya Covid-19 pamoja na maradhi yasiyoambukiza ambayo yanaongoza kwa kusababisha vifo vingi," alisema.

Mazrui alisema wananchi kuchukua kila aina ya tahadhari kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 ikiwamo kupunguza mikusanyiko ya wananchi isiyokuwa na sababu za msingi.

Alisema hivi karibuni imebainika kwamba idadi ya wagonjwa walioambukizwa na ugonjwa huo imeongezeka kutokana na kuwapo kwa mikusanyiko mingi inayotokana na sherehe za Maulidi ya kuzaliwa kwa kiongozi wa dini ya Kiislamu Mtume Muhammad.

Aliwataka wananchi kujitokeza kupata chanjo kujikinga na ugonjwa huo baada ya kubainika kuwapo mwitikio usioridhisha katika chanjo hiyo.

## Ashikiliwa tuhuma za kumeza kilo 1.5 heroin

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RASHID Habib Muhsin (53), anashikiliwa na polisi katika kitengo cha Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume baada ya kumeza jumla ya kete 101 za dawa za kulevya aina ya heroin akiwa katika hatua za mwisho kusafiri kwenda nchini Dubai.

Kaimu Kamishna wa Jeshi la Polisi kitengo cha Dawa za Kulevya Zanzibar, Omar Khamis, alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo wiki iliyopita baada ya kutiliwa shaka wakati akiwa katika jengo la abiria akisubiri ndege kuelekea Dubai.

Alisema mtuhumiwa alikuwa katika hatua za mwisho za kukamilisha safari yake kuelekea Dubai na ndipo alipotiliwa shaka na wafanyakazi pamoja na askari wa kitengo cha dawa za kulevya na kuchukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa awali.

"Tumefanikiwa kumkamata mtuhumiwa Rashid Habib Muhsini akiwa na dawa za kulevya amezimeza tumboni zenye uzito wa kilo moja na nusu na tunamshikilia kwa uchunguzi zaidi na ukikamilika tutamfikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili," alisema.

Aliwataka wananchi kuachana na biashara ya kusafirisha dawa za kulevya kwa kuwa Jeshi la Polisi liko makini.

# Serikali yaombwa ushirikiano wawekezaji wazalendo

Na Joseph Mwendapole

SERIKALI imeombwa kuwapa ushirikiano wawekezaji wazalendo waliowekeza kwenye sekta ya afya ili wawe endelevu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Hospitali ya KAM Musika, Dk. Kandore Musika, wakati wa ziara ya kutambulisha hospitali hiyo mwishoni mwa wiki Kimara Korogwe, jijini Dar es Salaam.

Dk. Kandore ni mwanzilishi wa KAM Dar es Salaam Pharmacy Limited, kampuni inayoendesha huduma za afya ikiwa na zahanati, hospitali, maduka ya dawa na Chuo cha Tiba cha KAM College of Health.

Dk. Kandore alisema wadau wengi walitaka kujua mambo mbalimbali kuhusu hospitali hiyo na aliamua kuwatengea siku hiyo kwa ajili ya kujionea yanayofanyika kwenye hospitali hiyo ambayo ilifunguliwa miezi miwili iliyopita.

Alisema Watanzania waliowekeza kwenye sekta ya afya wana moyo wa kusaidia wenzao kwa kuwa wawekezaji wengi kutoka nje wamewekeza kwenye miradi yenye faida na hawapendelei kuwekeza kwenye sekta ya afya.

Alisema yeye kama Mtanzania mzalendo atashukuru kama atapata msaada wa serikali kila inapopata fedha kutoka mataifa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya sekta ya afya.

Alisema misaada hiyo isielekezwe kwenye taasisi za serikali pekee kwa kuwa hata hospitali binafsi zinawahudumia mamilioni ya Watanzania wanapokuwa na matatizo.

"Hii ni taasisi ya familia na taasisi ya familia kwa Tanzania haiwezi kudumu miaka mingi hivyo serikali isipoangalia hii taasisi inaweza kupotea hivyo wakipata fungu kutoka kwa wafadhili watufikirie sisi wazalendo tuliowekeza kwenye sekta afya," alisema.

Dk. Musika alisema lazima kuwe na ushirikiano thabiti baina ya sekta ya umma na binafsi 'Public Private Partnership (PPP) kwa kuwa wote wanajenga nyumba moja, lakini kwa sasa hakuna ukaribu wa serikali kwenye kuwasaidia watu binafsi waliowekeza kwenye sekta ya afya.

"Hii ni taasisi kubwa ila hatuna uhakika baada ya miaka 20 kama KAM itabaki kuwa KAM ya leo hivyo serikali isipotuangalia hii hospitali inaweza isiwepo na isipokuwapo wananchi watapata shida sana, serikali iangalie hata namna ya kuingia ubia kwa kutuletea madaktari na mashine za vipimo mbalimbali, semina na kutuunganisha na wadau wa nje," alisema.

Alisema hospitali hiyo iko kwenye ngazi ya wilaya ikiwa na vitanda 122 na kuongeza kuwa kwa uhalisia ilipaswa kuanza kama hospitali ya Mkoa ila waliona ianze kwa ngazi ya wilaya na baada ya muda wataibadili iwe ya mkoa.

Alisema hospitali hiyo ina vipimo vya aina mbalimbali na wamepanga kuifanya iwe ya vipimo kwa kuhakikisha vipimo mbalimbali vinapatikana hospitalini hapo.

"Sisi hatuzingatii faida kwenye utoaji wa huduma zetu, tunatoa huduma kwa jamiii na lengo la hii hospitali ni kutoa huduma pia kwa wanafunzi wanaosoma hapa leo tunapanua wigo kushirikiana na wadau mbalimbali na itafuata miongozo yote ya wizara ya afya," alisema.

## Shinyanga yapokea tani 100 za mbegu

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

MKOA wa Shinyanga, umepokea tani 100 za mbegu za mahindi na alizeti kutoka kwa wakala wa mbegu za kilimo Agricultural Seed Agency (ASA), kwa ajili ya kuziuza kwa wakulima Kanda ya Ziwa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, akipokea mbegu hizo mwishoni mwa wiki, alisema zimekuja katika muda muafaka wa maandalizi ya msimu wa kilimo, na kuwataka wakulima wazitumie ili kufanya kilimo chenye tija na kupata mavuno mengi.

Alisema, maeneo mengi ya Mkoa wa Shinyanga yanakabiliwa na ukame na kwamba mbegu hizo ni mkombozi kwa mkulima, ambazo zikipandwa zinachukua muda mfupi kukomaa na kubainisha kwamba alizeti inachukua miezi minne na mahindi miezi mitatu.

"Tunashukuru kupata mbegu hizi bora kabisa za kilimo na naagiza sasa maofisa ugani muwatembelee wakulima huko maeneo ya vijijini na kuwapatia elimu ya kutumia mbegu hizi pamoja na kulima kisasa ili wapate mavuno mengi na kisha kuondokana na umaskini na baa la njaa hapo baadaye," alisema Mjema.

"Haiwezekani tumeletewa mbegu bora za kilimo, halafu mkoa wetu wa Shinyanga uje kutokea baa la njaa, hili sitakubali nataka tulime kimkakati ili tuwe na chakula cha kutosha," aliongeza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mbegu za Kilimo, Dk. Sophia Kashenge, alisema Mkoa wa Shinyanga wameuteua kuwa kituo kikuu cha kusambaza mbegu hizo za kilimo kwa Kanda ya Ziwa.

Alisema kwa upande wa mbegu za alizeti wameleta kilo 20,000, mahindi kilo 89,000, ambazo zinafikia tani 100.

Alisema katika mbegu za alizeti mkulima atauziwa kilo moja kwa Sh. 3,500, mahindi Sh. 2,700.



Muuguzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Vision Care Tanzania akifundisha wananchi wa Mlandizi mkoani Pwani, jinsi ya kutunza macho katika Kituo cha Afya cha Mlandizi kwa msaada wa Vision Care Tanzania na Korean International Cooperation Agency (KOICA) kabla ya kufanyiwa uchunguzi wa macho mwishoni mwa wiki. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

# NMB, Britam kuwezesha wavuvi bima maalum

Na Richard Makore, MWANZA

BENKI ya NMB kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Britam, wamezindua bima maalum ijulikanayo kama Jahazi kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Bima hiyo ilizinduliwa jana jijini hapa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki na inalenga kutoa nafasi kwa wavuvi kupata kinga wanapopata majanga mbalimbali.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mpozi, alisema bima hiyo inawalenga wavuvi wadogo na wa kati nchini.

Alisema wavuvi watakata bima ya asimilia tatu ya chombo husika cha shughuli ya uvuvi na wataweza kukingwa na majanga ya ajali, kuungua mitumbwi ama boti pamoja na watu watakaokuwa ndani ya vyombo hivyo.

Alliongeza kuwa faida nyingine za bima hiyo ni pamoja na familia ya mvuvi ama mtu aliyekuwa ndani ya chombo hicho kupewa mkono wa pole endapo kutatokea kifo pamoja na kupata ulemavu wa kudumu.

Vile vile, bima hiyo itatoa gharama za matibabu kwa mvuvi pamoja na kulipwa fidia kutokana na ajali yoyote itakayompata atakapokuwa majini kwa ajili ya shughuli za uvuvi ama kando kando ya ziwa, mto, bwawa ama bahari.

Aliwataka wavuvi kufika katika ofisi za NMB kwa ajili ya kukata bima ambayo itawakinga na majanga mbalimbali wanapokuwa katika shughuli zao kwenye maziwa, mito, mabwawa na bahari.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja wa Kampuni ya Bima ya Britam Kanda ya Ziwa, Said Kadabi, alisema, bima hiyo itawasaidia wavuvi kuinuka kiuchumi kwa kuwa sasa watafanya kazi zao kwa kujiamini.

Alisema wanalenga kuyafikia makundi mbalimbali ya kijamii na kuyakatia bima ikiwamo mama lishe ili waweze kufanya shughuli zao kwa kujiamini zaidi.

Kwa upande wake, Waziri Ndaki aliwataka wavuvi kutumia fursa hiyo kukata bima ili iwasaidie kuwakinga wanapokumbwa na majanga mbalimbali.

Alisema siku za nyuma bima ilikuwa inawaangalia wavuvi wakubwa pekee na sasa NMB na Britam wamekuja na aina mpya ya kuwasaidia wavuvi wadogo na wa kati.

Aliwataka wavuvi waendelee kupewa elimu ya bima ili waijue na kufanya uamuzi kwa kuwa ni njia sahihi ya kuwasaidia katika kipindi chote wanapokuwa katika shughuli zao.

Alisema NMB imedhamiria kuwainua kiuchumi wakulima, wafugaji na sasa ni zamu ya wavuvi na serikali inatambua mchango wao katika kuhakikisha makundi hayo yananufaika na mikopo inayotolewa na benki hiyo.

Alisema sekta ambazo zilikuwa zinaonekana kuwa na 'risk' kwa sasa zianze kufikiwa na kukatiwa bima kwa kuwa zina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

Waziri Ndaki alisema sekta ya uvuvi inaajiri watu milioni 4.5 na kwamba inachangia asilimia 1.7 ya pato la taifa na kwamba ni kundi muhimu ambalo linatakiwa kusaidiwa ili liweze kupiga hatua.

HABARI KIMATAIFA

## Xi aipuuzia Marekani uchunguzi chimbuko virusi vya corona

**Beijing, CHINA**

RAIS Xi Jinping wa China amepinga ombi la Marekani, kufanyika uchunguzi wa chimbuko la virusi vya corona.

Xi, amesema hayo wakati akitoa hotuba yake kwa njia ya mtandao kwenye mkutano uliokutanisha nchi 20, kwa nchi ambazo zimeendelea zaidi kiuchumi duniani, G20.

Wizara ya Mambo ya Nje ya China, ilisema Rais Xi aliuambia mkutano huo kwamba, China imetoa zaidi ya dozi bilioni 1.6 za chanjo ya virusi vya corona kwa mataifa na taasisi za kimataifa zaidi ya 100.

Aliongeza kwamba, China itatoa zaidi ya dozi bilioni mbili duniani katika mwaka huu.

Rais huyo wa China, alipendekeza kutoa msaada wa kifedha kwa ushirikiano wa chanjo duniani, ili kuruhusu nchi zinazoendelea kupata chanjo hizo.

Pia alisisitiza umuhimu wa kusaidia Shirika la Biashara la Kimataifa- Duniani (WTO) kufanya maamuzi mapema kwenye kuondoa haki miliki ya uvumbuzi kwenye chanjo za ugonjwa wa UVIKO-19.

Marekani, ilisema doa lililosababishwa na virusi na kufanya siasa za kufuatilia chimbuko la virusi, linakwenda kinyume na ari ya umoja dhidi ya janga hilo.

**NHK**

**Pia alisisitiza umuhimu wa kusaidia Shirika la Biashara la Kimataifa-Duniani (WTO) kufanya maamuzi mapema kwenye kuondoa haki miliki ya uvumbuzi kwenye chanjo za ugonjwa wa UVIKO-19.**

# Dunia yajadili kukabili ongezeko la joto

**Glasgow, SCOTALAND**

WAKUU wa mataifa mbalimbali duniani wamekutana kwa ajili ya mkutano wa tabianchi, mjini Glasgow, kujadili mipango ya kupunguza matumizi ya mafuta ya petroli, ili kuheshimu ahadi zao za kuilinda dunia.

Wakuu hao wamekutana kwenye mkutano ulioanza jana, hata hivyo bado hawakuweka sera zitakazozuia ongezeko la joto duniani, kuwa chini ya kiwango cha nyuzi joto mbili.

Hali hiyo, inachukuliwa kama mwendelezo wa kushindwa kutekeleza makubaliano waliyoyafikia katika mkutano wa kilele wa Paris Ufaransa miaka sita iliyopita, kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterress, aliandika kupitia ukurasa wake wa twitter kabla ya mkutano huo kwamba, iwapo serikali zote hasa za kundi la mataifa yanayoinukia na yaliyoendelea kiuchumi, G20, hayataweza kusimama na kuongoza juhudi za kupambana na mzozo wa kimazingira, dunia itaelekea kwenye mzozo mwingine mbaya wa kibinadamu.

Pamoja na onyo yanayotolewa na wanasayansi kuhusiana na utoaji wa hewa chafu, unaochangiwa na matumizi ya mafuta katika miaka ya hivi karibuni, imeshuhudiwa matukio mabaya ya mabadiliko ya hali ya hewa na maandamano ya wanafunzi, huku wanasiasa wakipuuzia mbali hayo.

Baada ya miongo miwili na nusu ya makubaliano, makumi kwa maelfu ya watu wanaelekeza macho yao Glasgow katika mkutano wa kimataifa wa mabadiliko ya tabianchi COP26.

Mkutano huo unatajwa kuwa tumaini pekee la mwisho la kusimamisha ongezeko la joto duniani.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, alisema kabla ya mkutano huo, kwamba wakati mambo yakianza kuharibika, yanaharibika kwa kasi ya ajabu," akifananisha mabadiliko ya tabianchi na anguko la uliokuwa utawala wa Roma.

Mikutano ya kilele ya Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, ni majukwaa ya watawala wa dunia ya kukubaliana kuhusu mipango ya kupunguza matumizi ya mafuta.

Zaidi ya makubaliano ya kiufundi, kama vile kanuni za mataifa kuripoti kuhusu namna yatakavyopunguza uchafuzi wa hewa ama watakavyofanikisha makubaliano yaliyopita, washiriki watajadiliana kuhusu masuala mawili muhimu, ikiamo usambazaji wa gesi chafu na fedha.

Uingereza ambayo ni mwenyeji wa mkutano huo inashinikiza viongozi kuahidi kupunguza usambazaji wa hewa ukaa kwa haraka zaidi. Imeyaweka masuala ya makaa ya mawe, magari, fedha taslimu na miti kama ajenda muhimu kwenye mkutano huo.

Mataifa tajiri yameshindwa kutimiza ahadi walizotoa kwenye mkutano kama huo uliopita wa kuyalipa mataifa maskini zaidi ya dola bilioni 100 kila mwaka, katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ifikapo mwaka 2020.

Baadhi ya wajumbe wa mataifa hayo maskini na yaliyo hatarini zaidi, ambao miongoni mwao wameshindwa kuhudhuria mkutano huo kutokana na vizuizi vya corona ama hali mbaya ya kifedha, wametoa wito kwa mataifa tajiri kulipia athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwa sababu ya kuchangia katika tatizo hilo kwa kiasi kikubwa.

Wanasayansi, wanaharakati na wajumbe wanaoongoza mapambano hayo, wanatilia shaka uwezo wa mikutano kama hiyo kusuluhisha matatizo huku wakiyakosoa mataifa tajiri kwa kushindwa kuheshimu ahadi zao.

Kabla ya makubaliano ya Paris, dunia ilikuwa ikielekea kuwa na ongezeko la joto la karibu nyuzi joto 4 C, iwapo ahadi zitatekelezwa, viwango hivyo vitaishia 2 C hadi 2.5 C ifikapo mwishoni mwa 2030.

**DW**



Baadhi ya viongozi duniani ambao nchi zao zina nguvu kiuchumi G20 wakiwa pamoja jana, kabla ya kushiriki mkutano kuhusu mabadiliko ya tabianchi COP26 jijini Glasgow, nchini Scotland. **PICHA: BBC**

# Watu wenye silaha wazuia muziki harusini

**Kabul, AFGHANISTAN**

WATU wenye silaha ambao walijitambulisha kama Wataliban, waliivamia harusi Mashariki mwa Afghanistan na kutaka muziki usipigwe.

Wapiganaji hao waliwaua watu wawili na wengine 10 kujeruhiwa, maofisa wameeleza.

Msemaji wa Taliban alisema wapiganaji wawili kati ya watatu wamekamatwa, ingawa wamekanusha wakidai zilikuwa wanatekeleza harakati za kiislamu.

Muziki ulipigwa marufuku wakati Taliban ilipoongoza mwaka 1996 mpaka mwaka 2001. Mamlaka mpya ya Taliban haijapitisha marufuku hiyo.

Shuhuda, aliiambia BBC, kulikuwa na ndoa za pamoja za wapenzi wanne katika wilaya ya Surkh Rod, Jimbo la Nangarhar Ijumaa, mwishoni mwa wiki.

Walipata ruhusa kutoka kwa viongozi wa eneo hilo wa Taliban, kucheza muziki katika eneo hilo ambalo lilikuwa linatumika na wanawake pekee.

Majira ya usiku, wapiganaji walivamia na kujaribu kuteketeza spika, huku wageni walipopinga wakimiminiwa risasi.

Msemaji wa Taliban, Zabihullah, alisema kesi hiyo bado inafanyiwa uchunguzi.

Kundi la wanamgambo wa kiislamu-IS ambao wanapingwa na Taliban, pia wanalaumiwa eneo lingine huko Nangarhar kwa tukio kama hilo kwa siku za nyuma.

Afghanistan, iliangukia utawala wa Taliban mwezi Agosti, mwaka huu, baada ya Marekani kuondoa majeshi yao katika nchi hiyo.

Wakati wa utawala wa awali, walikuwa wakiteleza sheria kali za kiislamu, sasa kuna mabadiliko kidogo na hata wanataka kutambuliwa kimataifa.

Tangu Taliban irudi madarakani, utawala huo umekuwa ukishutumiwa kufanya mauaji ya mwanamuziki na wanamuziki wengi wamekimbia nchi.

**DW**

# BANDA ATOA SABABU VIPIGO MTIBWA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kupata ushindi kwenye mechi ya tano mfululizo, huku ikichapwa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji juzi, beki wa Mtibwa Sugar, Hassan Banda, amesema timu yao ina tatizo la kushindwa kutumia nafasi wanazozipata, mawasiliano kati ya viungo na mabeki kuwa hafifu, lakini kutocheza kwenye uwanja halisi wa nyumbani.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam Jumamosi, Banda alisema tatizo kuu na la msingi la timu yao ni kushindwa kuzitumia nafasi wanazozipata.

"Unajua unapopoteza, kila mtu ataongea lake, tumeshindwa kuzuia sawa, lakini tunashindwa kutumia nafasi tunazozipata, ndiyo maana hata tukifungwa bao moja, inaonekana mabeki ndiyo wana matatizo," alisema beki huyo wa zamani wa Coastal Union na Simba.

Alisema sababu nyingine ni kwamba kuna wakati wanapoteza mawasiliano kati ya viungo na mabeki.

"Kwa mfano goli tuliofungwa, viungo walidhani ni faulo, wakaanza, wenzetu wakaendelea kucheza, wakafunga, hilo nalo ni tatizo," alisema.

Banda pia amebainisha kuwa kutokucheza kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Jamhuri Morogoro, pia kunachangia kutopata faida ya kucheza nyumbani.

"Unaona hii leo, tumecheza kwenye Uwanja wa Uhuru, huu ndiyo uwanja wetu wa nyumbani, wakati mwingine tunatumia Uwanja wa Mabatini, Mlandizi. Hakuna uwanja kamili wa nyumbani. Hili nalo pia tatizo," alisema.

Mtibwa Sugar imecheza mechi tano na kupata sare mbili, kufungwa tatu, hivyo kujikusanyia pointi mbili, ikishika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

## Usajili Kilimanjaro Marathon washika kasi

**Na Mwandishi Wetu**

MAANDALIZI kwa ajili ya mbio za kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager Marathon kwa mwaka wa 2022, yanaendelea vizuri huku usajili ukishika kasi mara tu baada ya kufunguliwa.

Hayo yamethibitishwa na waandaaji wa mbio hizo, ambapo wamebainisha kuwa punguzo la bei la asilimia 20 wakati wa kujisajili bado linaendelea.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa jijini Dar es Salaam jana, usajili bado unaendelea kufanyika kwa njia ya mtandao wa Tigopesa kwa kupiga *149*20#, pamoja na tovuti rasmi ya Kilimanjaro Marathon-www.kilimanjaromarathon.com.

Taarifa hiyo pia iliwakumbusha wanaotarajia kushiriki kutumia fursa ya muda wa punguzo gharama za kujisajili ambao ulianza Oktoba 17, mwaka huu, unatarajia kufikia kikomo Januari 7, mwakani.

"Baada ya muda wa punguzo kumalizika hakutakuwa na punguzo tena, badala yake washiriki watalazimika kulipa ada ya kawaida ya usajili," ilieleza na kusisitiza kuwa masuala yoyote kuhusu bei yanatangazwa kwenye kurasa maalumu tu za mtandao za Kilimanjaro Marathon na vyombo vya habari na si kwingineko.

Waandaaji hao wameendelea kutoa ushauri kwa wanaotarajia kushiriki mbio hizo kujiandikisha mapema ili waandaaji wapate nafasi ya kujitayarisha mapema zaidi.

"Usajili wa mapema pia utatupa sisi waandaaji nafasi ya kufanya matayarisho yanayohusiana na washiriki kama vile huduma za maji, magari ya wagonjwa, matunda na medali kwa vile tutakuwa na idadi yao mapema," ilielezea sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo pia imewakumbusha washiriki kuwa Kilimanjaro Premium Lager Marathon itaadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, jambo ambalo litakuwa tukio maalum, kubwa na la kipekee, hivyo ni vyema mtu akashiriki tukio hilo la kihistoria.

Wadhamini wa Kilimanjaro Premium Lager Marathon ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager - Km. 42, Tigo Kili Half Marathon - Km. 21na Grand Malt kilomita tano, ambapo wadhamini wa meza za maji kwa ajili ya washiriki ni Absa Tanzania, Unilever, Simba Cement, Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd, Kilimanjaro Water na TPC Sugar sambamba na watoa huduma maalumu ambao ni pamoja na GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel na CMC Automobiles.

Mbio za Kilimanjaro Marathon, zinazotarajiwa kufanyika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) Februari 27, mwakani, huandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Marathon na kuratibiwa kitaifa na Kampuni ya Executive Solutions.

**NAMNA HII...**



Straika wa Simba, Meddie Kagere, akiwa mazoezini juzi. Kulia kwake ni wachezaji wenzake, Bernard Morrison na Denis Kibu na kushoto ni Erasto Nyoni. Timu hiyo jana usiku iliikaribisha Coasta Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **MPIGAPICHA WETU**

## Kocha Biashara alia kucheza mfululizo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kulazimisha sare ya bao 1-1 siku ya Ijumaa dhidi ya Mbeya Kwanza FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Okumu, amesema kucheza mechi mfululizo kumesababisha uchovu kwa wachezaji wake.

Kocha huyo alisema mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara zimekuwa karibu mno, hivyo muda mrefu wamekuwa safarini kwenda kucheza badala ya kupumzika au kuwa mazoezini.

Jumanne iliyopita, Biashara United ilikuwa mjini Sumbawanga ikicheza dhidi ya Prisons na kuisulubu mabao 3-0 kabla ya Ijumaa kulazimisha sare ugenini dhidi ya Mbeya Kwanza FC.

"Mechi ilikuwa ngumu, tunashukuru kwa pointi moja, nadhani wachezaji wangu wamekuwa na uchovu sana kwa sababu mechi zimekuwa karibu karibu sana, vijana wamechoka. Lakini pamoja na hayo, hata Mbeya Kwanza ni timu nzuri sana na imepambana sana kwenye mechi hii," alisema Mkenya huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Haruna Hererimana, alisema: "Hakuna mechi nyepesi msimu huu. Tunashukuru hata kwa pointi hii moja tuliyoipata. Wachezaji wangu mwanzo walijisahau, hawakufuata maelekezo, tulipanga kwenye dakika 15 za kwanza tuwe tumepata goli, lakini badala yake dakika 13 za kwanza tukafungwa sisi".

## Wapya wawili KVZ kuivaa KMKM leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KVZ imepanga kuwatumia nyota wake wapya wawili katika mchezo wao wa leo dhidi ya Maafande wa KMKM, utakaopigwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri, imeeleza.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kocha Msaidizi wa KVZ, Ussi Ramadhani, alisema anatarajia kuwatumia Abubakar Ame "Luis" kutoka Mtibwa Sugar na Mohmed Ibrahim aliyejiunga na timu hiyo akitokea Chuoni FC.

Alisema katika mchezo huo lazima achukue tahadhari kwa kuwachezesha wachezaji wenye uzoefu ili kupata matokeo mazuri dhidi ya KMKM.

"KMKM tunajua ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu na wanakikosi kizuri, hivyo tunahitaji kuchukua tahadhari kubwa katika mechi hizi za mwanzo wa ligi kwa kuwa kila timu inahitaji kupata ushindi wa mapema," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**KROOS ATAKIWA NEWCASTLE**
NEWCASTLE imeonyesha nia ya kumtaka kiungo wa Real Madrid na Ujerumani, Toni Kroos mwenye umri wa miaka 31. **(El Nacional)**

**CONTE HATAKI TIMU**
ANTONIO Conte hataki kuchukua majukumu ya kuinoa timu katikati ya msimu. Kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Inter amekuwa akihuishwa na mpango wa kuchukua mikoba kule Manchester United na Newcastle United**. (Todofichajes)**

**HAG KUNG'OLEWA AJAX**
NEWCASTLE inamtaka kocha wa Ajax, Erik ten Hag kuwa kocha wao mpya, lakini wana wakati mgumu wa kumshawishi**. (Mirror)**

**JOVIC ATAKIWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL inafikiria kumsajili straika wa Real Madrid na Serbia, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 23. **(Fichajes)**

**KARIUS KUONDOKA ANFIELD**
LIVERPOOL watamwachia golikipa wao, Loris Karius mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ujerumani Januari akiwa hajaichezea klabu hiyo tangu 2018. **(Mirror)**

**BAYERN, SPURS KWA KOLO**
KLABU ya Tottenham Hotspur inakabiliwa na ushindani kutoka Bayern Munich kwenye mbio za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Nantes, Randal Kolo Muani, mwishoni wa msimu huu. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. **(Foot Mercato)**

**DE BEEK ABADILISHA WAKALA**
WACHEZAJI wenzake na Donny van de Beek pale Manchester United wamemshauri kubadilisha wakala wake ili aweze kuondoka hapo Old Trafford. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 anatajwa kuwaniwa na Everton na Wolves. **(Mail)**

**BARNES ATAKIWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL inafikiria kumsajili winga wa Leicester na England, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 23. **(Fichajes)**

**TOMAS AWINDWA TOTTENHAM**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeingia kwenye mbio moja na Leeds kuwania kumsajili straika wa Espanyol, Raul de Tomas mwenye umri wa miaka 27. **(Sport Witness, via TEAMtalk)**

**RAMSEY ATAJA NEWCASTLE**
NEWCASTLE haijakubaliana na matakwa ya mshahara unaotakiwa na Aaron Ramsey wakati wakifikiria kumsajili kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Wales kutoka Juventus kwenye dirisha la Januari. **(Tuttosport, via Mirror)**

**DERBY KUMUUZA MARSHALL**
KLABU ya Derby inataka kumuuza golikipa wake, David Marshall mwenye umri wa miaka 36 raia wa Scotland, Januari. **(Sun)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ASHUSHA PUMZI USHINDI UNITED KWA SPURS

**●●●Kazi yangu ni kuisaidia timu kutokana na uzoefu wangu, kwa mabao na asisti, na nilifanya hivyo, tulikuwa...**

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo amekisifu kiwango cha Manchester United wakati wakimpa ushindi mzuri kocha wao, Ole Gunnar Solskjaer kwa kuifunga Tottenham Hotspur mabao 3-0, juzi Jumamosi

Wakati Spurs sasa wakiwa kwenye matatizo yao, United walimpunguzia presha Solskjaer ambaye alionekana kuwa kwenye wakati mgumu kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.

Ronaldo alianza kwa kuiweka mbele United katika dakika ya 39, na nyota huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, alifanya kazi vizuri kumsaidia Edinson Cavani aliyefunga bao la pili, huku Marcus Rashford aliyetokea benchi akitupia la tatu.

Huo ulikuwa ushindi mkubwa zaidi kwenye ligi kwa United dhidi ya Tottenham tangu Februari 2007, wakati waliposhinda 4-0 pale kwenye dimba la White Hart Lane.

Na katika mchezo huo mwaka 2007, Ronaldo pia ndiye aliyefunga bao la kwanza kwa United wakati alipokuwa akicheza hapo.

Wikendi iliyopita Man United walifungwa mabao 5-0 nyumbani na Liverpool na kulikuwa na presha kubwa kuhusu mustakabali wa Solskjaer.

Ronaldo aliiambia Sky Sports: "Tulijua kabla ya mchezo kwamba tulikuwa na wiki ngumu.

"Tulikuwa na matokeo ambayo hatukuyatarajia. Timu ilikuwa kwenye presha kubwa, matokeo mabaya, lakini tulijua kwamba, leo (juzi) tunatakiwa kutoa jibu zuri. Tulicheza soka vizuri na kwa hakika ulikuwa mchezo mzuri.

"Kazi yangu ni kuisaidia timu kutokana na uzoefu wangu, kwa mabao na asisti, na nilifanya hivyo.

"Kwa upande wa timu ilikuwa kwenye kiwango bora kabisa kwa mtazamo wangu."

MECHI KALI

HOME

AWAY



WOLVERHAMPTON

2.22 | 3.20 | 3.35

EVERTON



KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa | vodacom | m-pesa | halopesa | airtel money | ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#


GBT:0249 18+

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# DE BEEK AMTEMA WAKALA WAKE



**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Donny de Beek, anaripotiwa kuwa ameamua kubadili wakala, na kuajiri wakala mpya katika jitihada zake za kujaribu kuondoka hapo Old Trafford.

Nyota huyo raia wa Uholanzi, ameendelea kuwa na kipindi kigumu pale Old Trafford akikosa muda wa kutosha wa kucheza.

Taarifa zinasema nyota huyo anapania kuondoka United kwenye dirisha la Januari, na amepokea ushauri na kuufanyia kazi kutoka kwa wenzake juu ya kuwa na wakala mpya.

Ripoti zinasema De Beek ameungana na Ali Dursun kwa sasa, akitarajia kazi nzuri ya kumwondoa klabuni hapo.

Klabu za Everton na Wolverhampton Wanders zinaripotiwa kuwa zipo tayari kumchukuwa kwa mkopo kwenye dirisha la uhamisho la Januari.

De Beek amecheza mechi tatu tu kwa michuano yote msimu huu akiwa chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer, akibahatika kucheza dakika sita pekee kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

# Aguero hali mbaya Barcelona



**BARCELONA, Hispania**

SERGIO Aguero alilazimika kukimbizwa hospitali baada ya kupata matatizo ya kifua wakati Barcelona wakitoka sare dhidi ya Alaves kwenye mchezo wao wa kwanza tangu kufukuzwa kwa kocha Ronald Koeman, Jumamosi.

Aguero alianguka na kushikilia kifua chake na alipatiwa huduma ya haraka uwanjani hapo kabla ya kutolewa uwanjani kuelekea kipindi cha pili.

Taarifa ya Barcelona baadaye ilisema kwamba alikimbizwa hospitali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kifua chake.

Luis Rioja aliisawazishia Alaves baada ya Memphis Depay kuwaweka mbele Barcelona kwa bao la mapema.

Strika huyo wa zamani wa Manchester City, Aguero mwenye umri wa miaka 33, alichukuliwa na gari la wagonjwa na kocha wa muda wa Barca, Sergi Barjuan aliiambia televisheni ya LaLiga: "Siwezi kusema mengi kwa sasa. Ninachojua amekimbizwa hospitali kwa ajili ya uchunguzi zaidi."

Raia huyo wa Argentina alikuwa ameanza mchezo wake wa kwanza kwenye kikosi hicho tangu alipojiunga nacho kipindi cha majira ya joto.

Aguero alijiunga Barca kwa mkataba wa miaka miwili baada ya kucheza kwa miaka 10 kule Man City, ambapo aliweka rekodi ya kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo akitikisa nyavu mara 260 kwenye mechi 390.

Pointi hiyo moja imeifanya Barcelona ishike nafasi ya tisa kwenye msimamo, ikipitwa pointi nane na vinara, Sevilla wenye alama sawa na Real Madrid, ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Elche, mapema Jumamosi.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY



# GUARDIOLA AKERWA NA KADI YA LAPORTE

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, hakuwa na furaha na maamuzi ya kumtoa nje kwa kadi nyekundu Aymeric Laporte na kukataliwa kwa bao la Gabriel Jesus wakati timu yake ikichezea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Crystal Palace.

Wilfried Zaha alifunga bao la mapema kabla ya Laporte kuonyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa kumdondosha mshambuliaji huyo wa Ivory Coast eneo la hatari.

Jesus alifunga bao la kuisawazishia City, lakini lilikataliwa na VAR kwa madai kwamba aliotea kabla ya Conor Gallagher kufunga la pili na kufanya matokeo kuwa 2-0.

Guardiola, ambaye alishindwa kupata ushindi kwenye mchezo wake wa 200 kwenye Ligi Kuu, alielezea kutoridhishwa kwake na maamuzi yaliyofanyika kwenye mchezo huo.

"Mambo mengi yalikwenda vibaya," alisema Guardiola akiiambia BBC baada ya mchezo huo.

"Tuliruhusu bao la mapema, na kipindi cha kwanza tulicheza vizuri, lakini wakati huo huo mwamuzi akamtoa mchezaji wetu nje.

"Mashabiki walikuwa nyuma yetu, lakini bahati mbaya bao letu likakataliwa. Mchana ule tukio kama lile lililofanywa na Jonny Evans wa Leicester City dhidi ya Arsenal, alionyeshwa kadi ya njano.

"Lakini sisi kwetu ilikuwa kadi nyekundu. Maamuzi ya kadi yanaonekana kuwa ni ya mwamuzi mwenyewe."

# Liver yafikiria kumsajili Jovic

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wametajwa kuwa wamemtambua kiungo wa Real Madrid, Luka Jovic kama lengo lao la usajili kwa dirisha la usajili la Januari.

Kwa hali ya sasa pale Liverpool, klabu haina uhakika juu ya kuendelea kuwapo kwa baadhi ya wachezaji, na hivyo wanahitaji kuweka mambo sawa kwa mipango ya mapema.

Pia kwa kuzingatia ratiba ya michuno ya mataifa ya Afrika (AFCON), ambayo imepangwa kuanza Januari 2022, Liverpool wapo kwenye hatari ya kukosa huduma ya wachezaji muhimu.




Kwa mujibu wa Fichajes, Liverpool wanaonekana kuwa na mpango wa kumsajili Jovic, ambaye kwa sasa anaonekana kukosa ushawishi kule kwenye dimba la Bernabeu.

Juzi Jumamosi kwenye mechi dhidi ya Elche, Jovic aliendelea kuwa benchi licha ya Karim Benzema kuwa majeruhi.

Real Madrid wanaweza wakalazimika kuachana na nyota huyo ambaye walimsajili kwa euro milioni 60 mwaka 2019 akitokea Eintracht Frankfurt ya Ujerumani.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 01 - NOVEMBA 2021


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2173 | Benevento vs Brescia | 2.05 | 3.48 | 3.28 |
| 15:00 | 2965 | FK Loznica vs FC Rad | 1.96 | 3.12 | 3.70 |
| 15:00 | 5151 | Strommen vs Ullensaker/Kisa | 2.14 | 3.62 | 2.80 |
| 15:30 | 3050 | Aluminium Arak vs Persepolis FC | 4.23 | 3.42 | 1.75 |
| 17:00 | 2441 | Spal vs Perugia | 2.21 | 3.14 | 3.24 |
| 17:00 | 2722 | Frosinone vs Crotone | 2.03 | 3.33 | 3.48 |
| 17:00 | 2737 | Monza vs Alessandria | 1.54 | 3.94 | 5.71 |
| 17:00 | 3047 | Ternana vs Como | 1.84 | 3.54 | 3.94 |
| 17:00 | 4107 | Sporting Farense vs Penafiel | 2.07 | 3.23 | 3.42 |
| 17:00 | 5318 | Reggina vs Cittadella | 2.27 | 3.10 | 3.15 |
| 18:00 | 5678 | SC Dnipro 1 vs FC Minaj | 1.39 | 4.54 | 6.19 |
| 18:30 | 2160 | Al Masry Club vs Smouha Club | 2.85 | 3.20 | 2.43 |
| 18:30 | 3202 | UTA Arad vs Chindia Targoviste | 1.97 | 3.09 | 4.02 |
| 19:30 | 4099 | Academica vs Nacional Madeira | 2.59 | 3.18 | 2.59 |
| 20:00 | 1082 | Basaksehir vs Adana Demirspor | 2.07 | 3.45 | 3.30 |
| 20:00 | 1277 | Giresunspor vs Antalyaspor | 2.16 | 3.20 | 3.35 |
| 20:00 | 1403 | Adanaspor vs Altinordu | 1.85 | 3.67 | 3.47 |
| 20:00 | 1928 | Parma vs Vicenza | 1.66 | 3.74 | 4.73 |
| 20:00 | 2150 | Istra vs Lokomotiva Zagreb | 2.98 | 3.22 | 2.20 |
| 20:00 | 2325 | Pisa vs Ascoli | 1.88 | 3.44 | 3.89 |
| 20:00 | 2402 | Bursaspor vs Keciorengucu | 1.86 | 3.51 | 3.61 |
| 20:00 | 3112 | Sandnes Ulf vs Fredrikstad | 2.46 | 3.48 | 2.46 |
| 20:00 | 4154 | Ranheim vs Kfum Oslo | 1.67 | 4.03 | 3.94 |
| 20:00 | 4292 | Ham-Kam vs Raufoss | 1.39 | 4.85 | 5.81 |
| 20:00 | 4616 | Proleter vs Vojvodina | 2.84 | 3.28 | 2.26 |
| 20:00 | 5783 | Pafos FC vs Paeek | 1.45 | 4.55 | 6.14 |
| 20:00 | 5840 | Pordenone vs Cremonese | 3.23 | 3.13 | 2.21 |
| 20:15 | 3433 | Tenerife vs Burgos | 1.77 | 3.20 | 4.92 |
| 20:30 | 4420 | Rayo Vallecano vs Celta Vigo | 2.39 | 3.30 | 2.95 |
| 20:30 | 4495 | HB Koge vs Horsens | 4.05 | 3.66 | 1.72 |
| 21:00 | 1500 | AFC Eskilstuna vs IFK Varnamo | 3.29 | 3.49 | 2.13 |
| 21:00 | 2158 | Odense vs Aarhus | 2.39 | 3.31 | 2.82 |
| 21:00 | 2176 | Verl vs Osnabruck | 3.44 | 3.48 | 1.99 |
| 21:00 | 2524 | Degerfors vs IFK Goteborg | 2.70 | 3.37 | 2.31 |
| 21:00 | 2541 | Gais vs Norrby IF | 2.80 | 3.31 | 2.49 |
| 21:00 | 3419 | Mjallby vs Hammarby | 2.85 | 3.38 | 2.21 |
| 21:00 | 3955 | Halmstads BK vs AIK Football | 2.99 | 2.99 | 2.32 |
| 21:30 | 1230 | Rapid Bucuresti vs U Craiova SA | 2.18 | 2.99 | 3.48 |
| 22:00 | 1471 | Helmond Sport vs Almere City | 3.27 | 3.57 | 2.00 |
| 22:00 | 2104 | Sporting Braga vs Portimonense | 1.45 | 4.24 | 6.70 |
| 22:00 | 2217 | Jong Ajax vs Telstar | 1.89 | 3.86 | 3.37 |
| 22:00 | 3980 | Aalesunds vs IK Start | 1.40 | 4.72 | 5.78 |
| 22:15 | 3283 | Maribor vs Luka Koper | 1.96 | 3.46 | 3.32 |
| 22:45 | 2027 | Bologna vs Cagliari | 1.73 | 3.94 | 4.39 |
| 22:45 | 3358 | Valenciennes vs AJ Auxerre | 3.05 | 3.25 | 2.25 |
| 22:45 | 4601 | Sligo Rovers vs Longford Town | 1.32 | 4.64 | 7.73 |
| 22:45 | 5062 | St Patricks vs Bohemians FC | 1.70 | 3.57 | 4.34 |
| 23:00 | 1712 | Finn Harps vs Drogheda Utd | 2.17 | 3.17 | 3.08 |
| 23:00 | 3169 | Wolverhampton vs Everton | 2.22 | 3.20 | 3.35 |
| 23:00 | 3265 | Levante vs Granada | 1.99 | 3.40 | 3.80 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Novemba 1, 2021

Nipashe



Ronaldo ashusha pumzi ushindi United kwa Spurs UKURASA 21

HAPA MWISHO...



Beki wa Kati wa Yanga, Dickson Job, akijipanga kumdhibiti Iddi Nado wa Azam FC baada ya kumtoka Feisal Salum 'Fei Toto', kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mugalu anarejea Sakho, Lwanga...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya jana kuendelea kuwakosa nyota wake watatu wa kikosi cha kwanza, Simba imetoa taarifa ya hali ya majeruhi kikosini mwao huku ikieleza muda si mrefu mshambuliaji wao, Chris Mugalu atarejea uwanjani.

Jana Simba iliikaribisha Coastal Union katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku nyota wake watatu; Mugalu, kiungo mshambuliaji Pape Sakho na kiungo mkabaji Taddeo Lwanga wakiendelea kukosekana kutokana na kuwa nje wakiuguza majeraha.

Lakini kwa mujibu wa taarifa ya Simba, wachezaji hao wanaendelea vizuri, na Mugalu ndiye anayeweza kurejea hivi karibuni kabla ya Sakho na Lwanga.

Mugalu ambaye aliumia kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga, hajacheza mchezo wowote wa Ligi Kuu msimu huu, wakati Sakho yeye mechi yake ya mwisho ilikuwa dhidi ya Dodoma Jiji FC, ambayo hakumaliza dakika 90 kutokana na kuumia.

Kwa upande wa Lwanga, aliumia katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na kuumia kwake kulichangia safu ya kiungo kupwaya na Simba kuangukia kichapo cha mabao 3-1 katika mechi hiyo ya marudiano iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# NABI ATANGAZA SOKA 'SAMBUSA' BADO YANGA

### ●●●Asema linaloonyeshwa kwa sasa ni asilimia 45 hadi 50 tu, aomba mwezi mmoja kufunika Ligi Kuu kwa...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Azam FC huku ikionyesha kandanda safi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anahitaji muda wa mwezi mmoja ili timu yake kuwa tishio zaidi katika michuano iliyopo mbele yao kwani wanachokionyesha kwa sasa ni asilimia 45 hadi 50 pekee.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Yanga ikiwa mwenyeji ilipata ushindi huo kupitia kwa Fiston Mayele na Jesus Moloko, hivyo kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo baada ya kufikisha pointi 12 ilizozikusanya kutokana na michezo minne iliyocheza hadi sasa na kupachika nyavuni jumla ya mabao sita huku ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikiswa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema ingawa wanapata matokeo mazuri na ushindi, lakini bado wachezaji hawajafikia malengo anayohitaji na kuomba muda wa mwezi mmoja ili kuendelea kukiimarisha kikosi chake.

Alisema kiwango kinachoonyeshwa na kikosi chake ni asimilia 45 hadi 50 tu, hivyo baada ya mwezi mmoja watafikia asilimia 100 sehemu ambayo anataka kuiona Yanga.

"Japokuwa tunapata matokeo mazuri, lakini bado timu yangu haijafikia yale malengo ninayohitaji kwa asilimia 100, kwa sasa wamefikia asilimia 45 hadi 50, nina matarajio makubwa baada ya mwezi mmoja na kuendelea Yanga itakuwa tishio na hatari kwa wapinzani," alisema Nabi.

Kuhusu ushindi walioupata, katika mechi dhidi ya Azam FC, alisema waliangalia kwanza udhaifu na ubora wa wapinzani wao na wakafanyia kazi na kufanikiwa kushinda mchezo huo.

"Azam FC si timu ndogo, ni timu kubwa, tulijiandaa kulingana na tulivyowaona wapinzani wetu, pia niwapongeze wachezaji wangu kupambana kupata pointi tatu," alisema Nabi.

Alisema matokeo hayo wanayapata kwa sababu ya usajili uliofanywa na uongozi kwa kuleta wachezaji aliowapendekeza, lakini kwa kocha wao wa viungo kufanya kazi kubwa ya kuwajenga kuwa fiti zaidi.

"Nampongeza kocha wa viungo kwani awali watu walikuwa wanamwongelea kuwa timu haiko fiti, lakini nataka niwaambie kwanza watu wafahamu yule ni dokta katika taaluma yake, muda ulikuwa mchache wa kujiandaa lakini leo (juzi) wenyewe mmeona," alisema.

Alisema kocha wa viungo amefanya kazi kubwa na kwamba licha ya kumaliza dakika 90 katika mchezo dhidi ya Azam, kikosi chake kilikuwa na uwezo wa kucheza dakika 30 nyingine bila kupumzika.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, aliwapongeza Yanga kwa mchezo mzuri kutokana na namna walivyocheza na kufafanua kuwa kwa upande wao walionekana kama hawapo uwanjani.

"Hatukuwa vizuri, ni kama hatukuwa uwanjani, hivyo kilicho mbele yetu sasa ni kuangalia michezo inayofuata ili kuona kama tutaweza kutimiza malengo yetu," alisema Bahati.

Alisema kwa matokeo hayo hakuna wa kulaumiwa kwa madai ya kuwakosa baadhi ya wachezaji kwani timu ina wachezaji 32, na hata kama wote wangekuwapo wasingeweza kuizuia Yanga kutokana na ubora waliouonyesha.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 12 baada ya kushuka dimbani mara nne ikishinda zote, lakini haijaruhusu nyavu zake kutikiswa hadi sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >